ISSN 0856-6976

# TAMKO LA SERA YA FEDHA

## *2025/26*

**BENKI KUU YA TANZANIA**

**Juni 2025**

ISSN 0856-6976

# TAMKO LA SERA YA FEDHA

## *2025/26*

**GAVANA**

**BENKI KUU YA TANZANIA**

Juni 2025

10 Juni 2025

**Mhe. Dkt. Mwigulu L. Nchemba (Mb),**
**Waziri wa Fedha,**
**Mji wa Serikali-Mtumba,**
**Barabara ya Hazina,**
**S. L.P 2802, 40468 Dodoma.**

Mheshimiwa Waziri,

**BARUA YA WASILISHO**

Kwa mujibu wa kifungu cha 21, kifungu kidogo cha (3) hadi (6) cha Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura ya 197, Benki inatakiwa kutoa **Tamko la Sera ya Fedha** mwezi Juni kila mwaka, likifuatiwa na tathmini ya nusu mwaka inayotolewa mwezi Februari. Tamko hili linaainisha mwelekeo wa sera ya fedha na utekelezaji wake katika kufikia malengo ya kiuchumi yaliyowekwa na Serikali. Kwa muktadha huo, nawasilisha kwako **Tamko la Sera ya Fedha kwa mwaka 2025/26**, kwa ajili ya kuwasilishwa Bungeni.

Tamko hili la Sera ya Fedha linatathmini mwenendo wa uchumi wa dunia na wa hapa nchini pamoja na utekelezaji wa sera ya fedha na matokeo yake kwa mwaka 2024/25. Aidha, Tamko hili linabainisha mwelekeo wa uchumi wa dunia na wa hapa nchini, pamoja na mwelekeo wa sera ya fedha kwa mwaka 2025/26. Vilevile, Tamko hili linaainisha sera ya riba pamoja na sera ya ubadilishaji fedha za kigeni ili kusaidia usimamizi wa uchumi nchini.

Wasalaam,

Emmanuel M. Tutuba
Gavana
Benki Kuu ya Tanzania

## YALIYOMO


**BARUA YA WASILISHO** .................................................... **i**
**MUHTASARI** .................................................... **iv**

**SEHEMU YA KWANZA** .................................................... **1**
1.0 UTANGULIZI .................................................... 1

**SEHEMU YA PILI** .................................................... **5**
2.0 MALENGO NA UTEKELEZAJI WA SERA YA FEDHA KWA MWAKA 2024/25 .................................................... 5
2.1 Malengo ya Sera ya Fedha .................................................... 5
2.2 Utekelezaji wa Sera ya Fedha .................................................... 5

**SEHEMU YA TATU** .................................................... **9**
3.0 MWENENDO WA UCHUMI WA DUNIA .................................................... 9
3.1 Ukuaji wa Uchumi wa Dunia .................................................... 9
3.2 Mwenendo wa Mfumuko wa Bei .................................................... 10
3.3 Mwenendo wa Bei za Bidhaa Katika Soko la Dunia .... 11
3.4 Mwenendo wa Masoko ya Fedha Duniani .................. 13

**SEHEMU YA NNE** .................................................... **15**
4.0 MWENENDO WA UCHUMI NCHINI .................................................... 15
4.1 Pato la Taifa .................................................... 15
4.2 Mfumuko wa Bei .................................................... 18
4.3 Mwenendo wa Ujazi wa Fedha na Mikopo kwa Sekta Binafsi .................................................... 22
4.4 Viwango vya Riba .................................................... 26
4.5 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali .................................................... 28
4.6 Deni la Taifa .................................................... 30

4.7 Mwenendo wa Sekta ya Nje .................................... 32
4.8 Ukwasi wa Fedha za Kigeni na Viwango vya Kubadilisha Fedha za Kigeni .................................... 39
4.9 Mwenendo wa Sekta ya Fedha .................................... 42
4.10 Mifumo ya Malipo .................................... 43

**SEHEMU YA TANO .................................... 49**
5.0 MATARAJIO YA HALI YA UCHUMI .................................... 49
5.1 Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia .................................... 49
5.2 Mwelekeo wa Uchumi wa Ndani .................................... 50

**SEHEMU YA SITA .................................... 53**
6.0 SERA YA FEDHA, RIBA NA UBADILISHAJI FEDHA ZA KIGENI 2025/26 .................................... 53
6.1 Mwelekeo wa Sera ya Fedha .................................... 53
6.2 Sera ya Riba .................................... 54
6.3 Sera ya Ubadilishaji Fedha za Kigeni na Akiba ya Fedha za Kigeni .................................... 54

VIAMBATISHO .................................... 56

# MUHTASARI

## Malengo na matokeo ya utekelezaji wa sera ya fedha kwa mwaka 2024/25

Sera ya fedha kwa mwaka 2024/25, ililenga kuhakikisha kuwa matarajio ya mfumuko wa bei yanabaki ndani ya lengo la asilimia 3 - 5, kuchagiza ukuaji wa uchumi kwa asilimia 5.4 kwa Tanzania bara na asilimia 7.2 kwa Zanzibar mwaka 2024, na kuhakikisha utulivu wa sekta ya fedha. Katika kufikia malengo haya, Benki Kuu ilipanga kutekeleza sera ya fedha kwa kutumia mfumo unaotumia riba ya Benki Kuu (CBR), ulioanza kutumika rasmi mwezi Januari 2024. Kwa muktadha huu, Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) ilikutana kila robo mwaka na kuamua riba ya Benki Kuu, huku utekelezaji wa sera ya fedha ukilenga kuhakikisha riba ya mikopo ya siku saba baina ya benki inabaki ndani ya wigo wa asilimia +/- 2 wa riba ya Benki Kuu.

Utekelezaji wa sera ya fedha ulikuwa wa kuridhisha, na hivyo kuwezesha kufikiwa kwa malengo ya uchumi kwa mwaka 2024/25. Riba ya Benki Kuu ilibaki kuwa asilimia 6, katika robo zote nne za mwaka 2024/25, ili kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei na kuchagiza ukuaji endelevu wa uchumi. Kiwango cha ukwasi kiliwiana na mahitaji ya shughuli za kiuchumi,hivyo kuchochea ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Riba ya mikopo ya siku saba katika soko la fedha baina ya benki ilikuwa tulivu na ndani ya wigo wa CBR, ingawa iliongezeka kidogo na kuvuka ukomo wa juu katika miezi ya Agosti, Septemba na Oktoba 2024. Mwenendo huu ulitokana na ongezeko la mahitaji ya fedha kwa ajili ya kununua mazao, kufuatia kiasi kikubwa cha mavuno, benki za biashara kuongeza uwekezaji katika rasilimali zilizo katika fedha za kigeni, na ongezeko la uwekezaji wa wananchi katika dhamana za Serikali na hivyo kupunguza amana zao katika benki za biashara. Kufuatia mwenendo

huu, Benki Kuu iliongeza ukwasi kwa kutumia nyenzo za sera ya fedha, ikiwemo utoaji wa mikopo ya muda mfupi kwa benki za biashara *(reverse repurchase agreements)*, kununua fedha za kigeni katika soko la jumla la fedha za kigeni na ubadilishanaji wa fedha za kigeni kwa shilingi na benki za biashara *(foreign exchange swap)*. Vilevile, Benki Kuu iliongeza ukwasi kupitia programu ya ununuzi wa dhahabu katika soko la ndani. Kufuatia hatua hizi, ukwasi katika uchumi uliongezeka na riba ya mikopo ya siku saba katika soko la fedha baina ya benki ilipungua na kuwa ndani ya wigo wa CBR.

**Mwenendo wa uchumi wa dunia**

Uchumi wa dunia uliimarika katika nusu ya pili ya mwaka 2024 kufuatia utekelezaji wa sera ya fedha iliyolenga kuongeza ukwasi kwenye uchumi, hatua za kuchagiza shughuli za kiuchumi zilizochukuliwa na serikali pamoja na ongezeko la matumizi ya walaji. Kufuatia mwenendo huu, Shirika la Fedha Duniani (IMF) linakadiria kuwa uchumi wa dunia ulikua kwa asilimia 3.3 mwaka 2024, ukilinganisha na asilimia 3.5 mwaka 2023. Takwimu za ukuaji wa uchumi wa dunia kwa nusu ya kwanza ya mwaka 2025 bado hazichapishwa. Hata hivyo, kwenye nchi zilizoendelea, hususan Marekani, ukuaji wa uchumi ulipungua katika robo ya kwanza ya mwaka 2025, kutokana na kutokutabirika kwa sera za biashara na kupungua kwa mahitaji ya walaji. Kwa upande wa nchi za Umoja wa Ulaya, takwimu za awali zinaonesha hali ya kuimarika kwa uchumi japo kwa kasi ndogo. Kasi ya ukuaji wa uchumi katika nchi za BRICS ilitofautiana baina ya nchi. Ukuaji wa uchumi nchini China, Urusi, Afrika Kusini na Brazili ulipungua kutokana na mivutano ya kibiashara, huku ukuaji nchini India ukiongezeka, kufuatia kuongezeka kwa mahitaji ya walaji, na uwekezaji katika ujenzi wa miundombinu na sekta ya kidijitali. Mfumuko wa bei duniani uliendelea kupungua, japo kwa kasi tofauti baina ya kanda, na hivyo kupelekea kupungua kwa

riba za sera ya fedha ili kuchagiza ukuaji wa shughuli za uchumi. Katika nchi zilizoendelea, hususan Marekani na Umoja wa Ulaya, mfumuko wa bei uliendelea kupungua kutokana na matokeo ya utekelezaji wa sera ya fedha na kupungua kwa bei za nishati.

Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, bei za bidhaa katika soko la dunia zilikuwa na mwenendo iliyotofautiana. Bei za dhahabu, kahawa, mbolea na tumbaku ziliongezeka, huku bei za mafuta ghafi, pamba na sukari zikipungua. Kupanda kwa bei za dhahabu kulitokana na mivutano ya kibiashara inayoendelea na hivyo kusababisha ongezeko la mahitaji ya dhahabu kama rasilimali salama ya uwekezaji na kuweka akiba. Bei ya kahawa *(Arabica na Robusta)* iliongezeka kutokana na matarajio ya kupungua kwa uzalishaji duniani. Aidha, kushuka kwa wastani wa bei za mafuta ghafi kulisababishwa na kupungua kwa mahitaji, na matokeo ya ongezeko kubwa la ushuru wa forodha. Bei za pamba zilishuka kutokana na kupungua kwa mahitaji duniani, wakati bei za sukari zilipungua kutokana na ongezeko la uzalishaji.

Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, masoko ya fedha duniani yaliathiriwa na mabadiliko ya sera za fedha, na kutotabirika kwa hali za kisiasa duniani. Nchini Marekani, riba za hati fungani za serikali ziliendelea kuwa juu, ambapo riba ya hatifungani ya miaka 10 ilikuwa kati ya asilimia 4.1 na asilimia 4.6, huku Benki Kuu nchini humo ikiendelea kuchukua tahadhari katika kupunguza viwango vya riba ya sera ya fedha. Katika nchi za umoja wa Ulaya, riba za hati fungani za serikali zilikuwa na mwenendo wa kubadilikabadilika. Nchini China, riba za hati fungani za serikali zilibaki kuwa za chini, ambapo riba ya hati fungani ya miaka 10 ilibaki kati ya asilimia 2.3 hadi asilimia 2.6, huku Benki Kuu ya China ikiendelea kutekeleza sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi kwenye uchumi kufuatia kupungua kwa mahitaji

ya ndani na mfumuko wa bei. Kuelekea Juni 2025, masoko ya fedha yanatarajiwa kuendelea kuathiriwa na taarifa za kiuchumi na maamuzi ya kisera, hususan katika Benki Kuu za nchi zilizoendelea.

**Mwenendo wa uchumi wa Tanzania**

Uchumi wa Tanzania Bara na Zanzibar ulikua kwa kasi ya kuridhisha mwaka 2024, ukichangiwa zaidi na uwekezaji unaoendelea kufanywa na Serikali na sekta binafsi. Kwa upande wa Tanzania Bara, uchumi ulikua kwa asilimia 5.5, juu ya asilimia 5.1 mwaka 2023. Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na shughuli za kilimo, ujenzi, fedha na bima, pamoja na shughuli za uchimbaji madini na mawe. Kwa upande wa Zanzibar, uchumi ulikua kwa asilimia 7.1 mwaka 2024, chini kidogo ya asilimia 7.4 mwaka 2023, kufuatia kukamilika kwa baadhi ya miradi mikubwa ya miundombinu na uwekezaji. Licha ya mwenendo huu, uchumi uliendelea kuwa imara ukichangiwa zaidi na shughuli za malazi na huduma za chakula, hususan kutokana na kuongezeka kwa shughuli za utalii.

Mfumuko wa bei umeendelea kuwa tulivu, ndani ya lengo la nchi na vigezo vya mtangamano wa kiuchumi kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Umoja wa Maendeleo wa Kusini mwa Afrika (SADC). Kwa upande wa Tanzania Bara, mfumuko wa bei ulikuwa wastani wa asilimia 3.1 katika miezi kumi ya kwanza ya mwaka 2024/25, kufuatia utekelezaji wa sera madhubuti ya fedha na kupungua kwa bei za bidhaa zisizo za chakula. Kwa upande wa Zanzibar, mfumuko wa bei ulipungua hadi wastani wa asilimia 5, kutoka asilimia 5.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24, kutokana na kupungua kwa bei za chakula.

Ujazi wa fedha uliendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha katika miezi kumi ya mwanzo ya mwaka 2024/25. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana

zaidi (M3) ulikua kwa wastani wa asilimia 13.8, ikilinganishwa na asilimia 14.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Mwenendo huu, ulichangiwa zaidi na mikopo kwa sekta binafsi, ambayo ilikua kwa wastani wa asilimia 15.1 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 18.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Mwenendo huu unaakisi utekelezaji wa sera ya fedha iliyolenga kudhibiti viashiria vya mfumuko wa bei kutokana na kupungua kwa thamani ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni.

Utekelezaji wa bajeti kwa Serikali zote mbili ulikuwa wa kuridhisha katika miezi kumi ya mwanzo ya mwaka 2024/25. Kwa upande wa Tanzania bara, mapato ya ndani yalifikia asilimia 99 ya makadirio, yakichangiwa zaidi na makusanyo ya kodi ambayo yalivuka lengo kufikia asilimia 102.2. Kwa upande wa Zanzibar, mapato ya ndani yalifikia asilimia 99.2 ya makadirio huku makusanyo ya kodi yakivuka lengo wa asilimia 3. Serikali ziliendelea kupanga matumizi kulingana na mapato.

Sekta ya nje imeendelea kuimarika licha ya migogoro ya kisiasa na mvutano wa kibiashara duniani. Katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, nakisi ya urari wa malipo ya kawaida ilipungua na kufikia dola za Marekani milioni 1,677.3 kutoka dola za Marekani milioni 2,219.8 kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Mwenendo huu, ulichangiwa zaidi na kuongezeka kwa mauzo nje ya nchi hususan, mapato ya utalii na dhahabu sambamba na kupungua kwa kasi ya ongezeko la uagizaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi. Kwa upande wa Zanzibar, ziada ya urari wa malipo ya kawaida iliongezeka hadi dola za Marekani milioni 719.1 ikilinganishwa na ziada ya dola za Marekani milioni 490.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24, ikichangiwa zaidi na ongezeko la mapato yatokanayo na utalii na kupungua kwa uagizaji wa bidhaa kutoka nje. Akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni

5,307.7 mwishoni mwa Aprili 2025, kiasi kinachotosha uagizaji bidhaa na huduma nje ya nchi kwa miezi 4.3, juu ya lengo la nchi la miezi 4.

Mwaka 2024/25, hali ya ukwasi katika soko la fedha za kigeni ilibadilika kuendana na mwenendo wa uchumi wa dunia pamoja na misimu ya mapato ya fedha za kigeni. Katika robo ya kwanza ya mwaka 2024/25, hali ya ukwasi wa fedha za kigeni ilipungua kufuatia changamoto zilizokumba uchumi wa dunia, japo iliimarika katika robo ya pili, sambamba na kuimarika kwa mazingira ya kiuchumi duniani, ongezeko la mapato ya fedha za kigeni kutokana na shughuli za utalii, pamoja na mauzo ya dhahabu, korosho, na tumbaku na utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha. Kwa robo ya tatu ya mwaka 2024/25, ukwasi katika soko la fedha za kigeni ulipungua kidogo, kufuatia kumalizika kwa msimu wa mauzo ya mazao nje ya nchi. Thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani ilibadilika kuendana na hali ya ukwasi wa fedha za kigeni nchini. Kwa wastani, kuanzia Julai 2024 hadi Aprili 2025, thamani ya Shilingi dhidi ya dola ya Marekani katika soko la jumla la fedha za kigeni ilipungua kwa wastani wa asilimia 4.7, ikilinganishwa na kupungua kwa wastani wa asilimia 7.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24.

Sekta ya fedha iliendelea kuwa imara na thabiti dhidi ya mitikisiko ya muda mfupi, huku viashiria vyote vya msingi vikiwa ndani ya viwango vinavyokubalika. Sekta ya benki ilikuwa na mtaji, ukwasi wa kutosha na yenye kutengeneza faida, huku ikiendelea kunufaika na mifumo ya kidijitali katika utoaji wa huduma. Uwiano wa mtaji kwa rasilimali (*core capital adequacy ratio*) ulikuwa asilimia 20.2, juu ya ukomo wa chini unaokubalika kisheria wa asilimia 10. Ubora wa rasilimali za benki uliendelea kuongezeka kufuatia kupungua kwa mikopo chechefu hadi asilimia 3.5 mwezi Aprili 2025, kutoka asilimia 4.1 mwezi Juni 2024, na chini ya kiwango kinachovumilika cha asilimia 5.

Mifumo ya malipo iliendelea kufanya kazi kwa ufanisi, ikiwa na kiwango cha upatikanaji cha zaidi ya asilimia 99. Benki Kuu imeendelea kufanya maboresho katika mifumo hiyo, hususan kwa kutekeleza awamu ya tatu ya Mfumo wa Malipo ya Papo Hapo (TIPS), na kwa kuhamia kwenye viwango vya ujumbe vya ISO20022. Hatua hizi zinalenga kuboresha ufanisi na uoanifu wa miamala ya ndani na ya kimataifa. Aidha, katika jitihada za kuongeza matumizi ya malipo ya kidijitali na kupunguza utegemezi wa fedha taslimu katika kufanya miamala, Benki Kuu imechukua hatua za ziada kwa kufanya maboresho ya ada za miamala inayofanyika kati ya mifumo oanifu (interoperable transactions), ikiwemo kutoka benki kwenda kwenye akaunti za simu za mkononi na kutoka akaunti za simu kwenda akaunti za benki, kupitia TIPS na hivyo kuongeza unafuu kwa watumiaji. Mifumo ya malipo ya kikanda, ikiwemo Mfumo wa Malipo wa Afrika Mashariki (EAPS) na Mfumo wa Malipo wa ya Papo kwa Hapo wa SADC (SADC-RTGS), iliendelea kufanya kazi vizuri na kuwezesha kufanyika kwa miamala ndani ya kanda husika. Ili kuongeza matumizi ya mifumo hii, Benki Kuu kwa kushirikiana na benki kuu za EAC na SADC, zimeendelea kutekeleza hatua mbalimbali za kuongeza matumizi ya mifumo hii. Vilevile, simu za mkononi zimeendelea kutumika katika kusaidia kufikisha huduma za kifedha kwa wananchi ambao hawajafikiwa na huduma za benki.

**Matarajio ya hali ya uchumi**

Uchumi wa dunia unatarajiwa kuwa na mwenendo usioridhisha, ambapo kasi ya ukuaji inatarajiwa kupungua japo kwa viwango tofauti baina ya nchi. Taarifa ya Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia *(World Economic Outlook - WEO)* iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) mwezi Aprili 2025, inakadiria ukuaji wa uchumi wa dunia kupungua hadi asilimia 2.8 mwaka 2025 na asilimia 3.0 mwaka 2026, kutoka makadirio ya asilimia 3.3 kwa miaka yote miwili, mwezi Januari

2025. Mwenendo huu unatokana na kuongezeka kwa mivutano ya kibiashara, kufuatia ongezeko kubwa la ushuru wa forodha kwa bidhaa na sintofahamu katika sera za kiuchumi na athari za ongezeko kubwa la riba.

Mfumuko wa bei duniani unatarajiwa kupungua, ingawa kwa kasi ndogo kuliko ilivyokadiriwa mwezi Januari 2025 na kufikia asilimia 4.3 mwaka 2025 na asilimia 3.6 mwaka 2026. Aidha, mfumuko wa bei kwa nchi zilizoendelea unakadiriwa kuwa juu kidogo mwaka 2025, kulinganishwa na makadirio ya awali, na chini ya makadirio ya awali kwa nchi zinazoendelea na zile zinazoibukia kiuchumi. Hata hivyo, mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kupungua kutokana na matokeo ya utekelezaji wa sera za fedha iliyolenga kupunguza ukwasi katika nchi nyingi pamoja na mwenendo wa bei za bidhaa muhimu kama chakula na nishati katika soko la dunia. Kwa muktadha huo, benki kuu za nchi nyingi zilizoendelea hususan Marekani na Ulaya zinatarajiwa kuweka kipaumbele katika kuchochea ukuaji wa uchumi, hatua inayoweza kupelekea kupunguza riba zao za sera ya fedha.

Uchumi wa hapa nchini unatarajiwa kuendelea kuimarika, licha ya mvutano wa kibiashara unaoendelea duniani. Kwa upande wa Tanzania Bara, uchumi unatarajiwa kukua kwa asilimia 6 mwaka 2025 na asilimia 6.3 mwaka 2026. Mwenendo huu utachagizwa na uwekezaji katika sekta ya umma hususan katika ujenzi wa miundombinu kama reli, barabara, viwanja vya michezo na viwanja vya ndege. Vilevile, uwekezaji katika sekta ya kilimo, hususan miradi ya umwagiliaji, pamoja na hali nzuri ya hewa na sera wezeshi utachochea ukuaji wa sekta hii. Uchumi wa Zanzibar unatarajiwa kukua kwa asilimia 6.5 mwaka 2025 na asilimia 6.7 mwaka 2026, ukichangiwa zaidi na shughuli za ujenzi wa miundombinu kama barabara, bandari na majengo pamoja na ongezeko la shughuli za viwanda na utalii.

Mfumuko wa bei unatarajiwa kubaki ndani ya lengo la muda wa kati la asilimia 3-5, ukichangiwa na upatikanaji wa chakula cha kutosha, nishati ya uhakika ya umeme na utekelezaji wa sera madhubuti za fedha na za bajeti. Aidha, uwezekano wa kupanda kwa mfumuko wa bei ni mdogo, japo mwenendo huu unaweza kuathiriwa na kuongezeka kwa mvutano wa kibiashara au migogoro katika eneo la Mashariki ya Kati.

**Mwelekeo wa sera ya fedha 2025/26**

Kulingana na matarajio ya mwenendo wa uchumi pamoja na athari zilizoainishwa, Benki Kuu inatarajia kutekeleza kwa tahadhari sera ya fedha yenye lengo la kuongeza ukwasi kwenye uchumi mwaka 2025/26. Lengo ni kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki ndani ya lengo la asilimia 3-5, sambamba na kuwezesha kufikiwa ukuaji wa uchumi wa asilimia 6 mwaka 2025 na asilimia 6.3 mwaka 2026 kwa Tanzania Bara, na asilimia 6.5 na asilimia 6.7 kwa Zanzibar, mtawalia. Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) itakutana kila robo mwaka, kutathmini hali uchumi na mwelekeo wake, na kuamua kiwango cha Riba ya Benki Kuu (CBR) kitakachoendana na malengo ya mfumuko wa bei na ukuaji wa uchumi.

Katika kuboresha maamuzi ya sera ya fedha kwa kuzingatia takwimu, Benki Kuu itaendelea kufanya tafiti mbalimbali na kuhakikisha upatikanaji wa takwimu bora. Tafiti zitakazofanyika zitalenga kuongeza ufanisi wa sera ya fedha. Vilevile, Benki Kuu itaendelea kuelimisha wananchi kuhusu mfumo wa sera ya fedha unaotumia riba ya Benki Kuu, pamoja na umuhimu wa matumizi ya Shilingi katika miamala inayofanyika hapa nchini, ili kuongeza ufanisi wa sera ya fedha katika kufanikisha utulivu wa bei na kuchochea ukuaji wa uchumi. Pamoja na hayo, Benki Kuu itaendelea kufanya maboresho kadhaa yenye lengo la; (i) kuongeza uthabiti wa sekta ya fedha na kupunguza vihatarishi vinavyoambatana na utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi, (ii) kuongeza

huduma jumuishi za kifedha (kuongeza ufikiwaji wa huduma za kifedha, kuongeza wigo wa huduma za kifedha, kuongeza ufanyaji wa malipo kwa njia za kidijitali, kuendelea kutoa elimu ya masuala ya fedha kwa wananchi na kumlinda mteja wa huduma za kifedha), na (iii) kuongeza ukwasi na ufanisi wa masoko ya fedha. Vilevile, Benki Kuu itaendelea kufanya maboresho katika mfumo unaotumika kufanya maoteo ya kiwango cha ukwasi nchini na kuchukua hatua za kuongeza uwazi na kupunguza vihatarishi vya ukopeshaji katika soko la fedha baina ya benki, ili kuhakikisha kuwa riba ya mikopo ya siku saba katika soko la fedha kati ya benki inabaki ndani ya wigo wa asilimia +/- 2 ya riba ya Benki Kuu.

**Sera ya riba**

Viwango vya riba vitaendelea kuamuliwa kwa nguvu za soko ili kuongeza ufanisi katika upatikanaji wa mitaji hapa nchini. Maamuzi ya Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) kuhusu Riba ya Benki Kuu (CBR) yanategemewa kuongoza upangaji wa riba za mikopo na huduma nyingine za kifedha. Aidha, Benki Kuu kwa kushirikiana na wadau wengine, itaendelea kufanya maboresho katika sekta ya fedha ili kuongeza uwazi katika upangaji wa riba, sambamba na kuongeza usimamizi wa benki na taasisi za huduma ndogo za kifedha, kuongeza wigo wa huduma za kifedha na kutoa elimu ya masuala ya kifedha na upatikanaji wa taarifa kwa wananchi.

**Sera ya ubadilishaji fedha za kigeni na akiba ya fedha za kigeni**

Kiwango cha ubadilishaji wa fedha za kigeni kitaendelea kuamuliwa na uwiano wa mahitaji na upatikanaji wa fedha za kigeni katika soko, na hivyo kutumika kama kinga ya uchumi dhidi ya athari zitokanazo mitikisiko ya uchumi duniani. Kwa mantiki hii, Benki Kuu itashiriki

katika soko la jumla la fedha za kigeni kwa mujibu wa Sera ya Ushiriki wa Soko la Fedha za Kigeni, kwa lengo la; kupunguza mabadiliko makubwa ya muda mfupi katika kiwango cha ubadilishaji wa fedha, kuongeza akiba ya fedha za kigeni, kufanikisha utekelezaji wa sera ya fedha, na kuongeza ukwasi wa fedha za kigeni katika soko. Benki Kuu pia, itaendelea kuhakikisha washiriki wote katika soko la fedha za kigeni wanazingatia kanuni, miongozo na maadili ya ushiriki katika soko hili. Ili kulinda uthabiti wa thamani ya Shilingi, Benki Kuu itaendelea kuhakikisha uwepo wa akiba ya kutosha ya fedha za kigeni, inayotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa angalau miezi minne kwa mwaka 2025/26. Hii itafanyika kupitia mikakati ya kuongeza akiba ya fedha za kigeni, ikiwemo, mpango wa Benki Kuu wa ununuzi wa dhahabu katika soko la ndani, pamoja na kuingia mikataba ya kubadilishana fedha za kigeni kwa shilingi *(foreign exchange swaps)* pale itakapobidi.

# SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

Tamko la Sera ya fedha kwa mwaka 2024/25 lililochapishwa na Benki Kuu ya Tanzania mwezi Juni 2024 liliainisha malengo ya sera za kiuchumi kwa mwaka 2024/25 kama yalivyoainishwa katika Mipango ya Maendeleo ya Taifa. Malengo haya yalizingatia mwenendo wa uchumi wa dunia na wa hapa nchini. Malengo hayo yalikuwa ni; (i) kufikia ukuaji wa uchumi wa asilimia 5.4 kwa mwaka 2024 na asilimia 6 kwa mwaka 2025 kwa Tanzania Bara na ukuaji wa asilimia 7.2 na asilimia 6.8, kwa Zanzibar, mtawalia na (ii) kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki ndani ya lengo la asilimia 3-5 mwaka 2024/25 kwa Tanzania Bara na Zanzibar.

Tamko hili la Sera ya Fedha la mwaka 2025/26 linatathmini utekelezaji wa sera ya fedha na matokeo yake kwa mwaka 2024/25, pamoja na mwenendo wa uchumi wa dunia na hapa nchini. Vilevile, Tamko hili linatoa mwelekeo wa uchumi wa dunia na wa hapa nchini, na sera ya fedha kwa mwaka 2025/26.

Pamoja na Sehemu hii ya Utangulizi, Tamko hili limepangwa kwa mtiririko ufuatao: Sehemu ya Pili inaainisha malengo na matokeo ya utekelezaji wa sera ya fedha kwa mwaka 2024/25. Sehemu ya tatu inachambua mwenendo wa uchumi wa dunia, ikifuatiwa na Sehemu ya Nne inayotathmini mwenendo wa uchumi wa hapa nchini. Sehemu ya Tano inatoa mwelekeo wa uchumi wa dunia na wa hapa nchini na Sehemu ya Sita inahitimisha kwa kutoa mwelekeo wa sera ya fedha pamoja na sera za riba na viwango vya ubadilishaji wa fedha za kigeni zitakazotekelezwa na Benki Kuu ya Tanzania kwa mwaka 2025/26 ili kufikia malengo yake.

### Mfumo wa Sera ya Fedha wa Benki Kuu ya Tanzania

Mfumo wa sera ya fedha ya Benki Kuu ya Tanzania hulenga kudhibiti mfumuko wa bei nchini na kuwezesha ukuaji endelevu wa uchumi. Mnamo mwezi Januari 2024, Benki Kuu ilianza rasmi kutekeleza sera ya fedha kwa kutumia mfumo wa riba ili kuongeza ufanisi, sawia na mabadiliko ya mazingira ya kiuchumi. Mfumo huu ambao unazingatia zaidi mwelekeo na matarajio ya mwenendo wa viashiria mbalimbali vya kiuchumi (*forward looking*) hutumia riba ya Benki Kuu ili kuchagiza mwenendo wa riba za muda mfupi katika masoko ya fedha, ambazo hutarajiwa kuashiria viwango vya riba vya muda mrefu na hatimaye kuelekeza mfumuko wa bei na ukuaji wa uchumi. Mambo muhimu katika mfumo wa sera ya fedha unaotumia riba ya Benki Kuu yameainishwa kama ifuatavyo.

### Lengo la Sera ya Fedha

Lengo la msingi la sera ya fedha ni kuhakikisha utulivu wa bei, yaani kiwango kidogo na thabiti cha mfumuko wa bei. Mfumuko wa bei hupimwa kwa kuangalia mabadiliko ya kila mwaka katika fahirisi za bei za walaji nchini ambalo huwasilishwa kwa asilimia. Mfumuko wa bei unatarajiwa kuwa asilimia 3-5 katika muda wa kati. Lengo hili ni muafaka kwa ajili ya kuchochea ukuaji endelevu wa uchumi nchini, pamoja na kuhakikisha utulivu wa riba na thamani ya shilingi ya Tanzania dhidi ya sarafu za nchi nyingine.

### Lengo la Kati

Benki Kuu inadhibiti mfumuko wa bei na kuwezesha ukuaji wa uchumi kwa kupanga Riba ya Benki Kuu (CBR). Riba hii hupangwa kuendana na maoteo ya mfumuko wa bei, sambamba na ukuaji endelevu wa uchumi.

### Kiashiria cha Utendaji

Chini ya mfumo wa sera ya fedha unaotumia riba, Benki Kuu inahakikisha kuwa riba ya mikopo ya siku 7 katika soko la fedha baina ya benki (lengo la uendeshaji) inaendana na riba ya Benki Kuu ili kufikia malengo ya

mfumuko wa bei na ukuaji wa uchumi. Riba ya siku 7 katika soko la fedha baina ya benki imechaguliwa na Benki Kuu kwa kuwa ni tulivu na ina uhusiano wa karibu na riba ya Benki Kuu.

**Nyenzo za Sera ya Fedha**

Benki Kuu ya Tanzania inatumia nyenzo mbalimbali za sera ya fedha ili kuhakikisha kuwa lengo la uendeshaji linaendana na riba ya Benki Kuu. Nyenzo kuu za utekelezaji wa sera ya fedha ni pamoja na mikopo ya muda mfupi baina ya Benki Kuu na benki za biashara (*repurchase agreement and reverse repurchase agreement*). Nyenzo nyingine ni uuzaji na ununuzi wa dhamana *(open market operations*), na uuzaji na ununuzi wa fedha za kigeni katika soko la jumla la fedha za kigeni baina ya benki. Nyenzo nyingine zinazotumika ni pamoja na kiwango cha amana za benki za biashara kinachotakiwa kuwekwa kisheria Benki Kuu (*Statutory Minimum Reserve*) na riba inayotumika kutoza benki au Serikali zinapochukua mikopo Benki Kuu. Pamoja na nyenzo hizo, Benki Kuu pia inatoa mikopo ya muda mfupi ambayo hutakiwa kurudishwa ndani ya siku husika na ile ya siku moja (*Intraday and Lombard loan facilities*) ili kusaidia uwepo wa ufanisi katika mifumo ya malipo na ufanyaji wa miamala. Aidha, Benki Kuu inaweza kutumia nyenzo nyingine za sera ya fedha kuendana na mahitaji ili kufanikisha kufikiwa kwa malengo ya kisera.

## Uwasilishaji wa Sera ya Fedha kwa Umma

Benki Kuu ya Tanzania inatekeleza jukumu lake la uandaaji na utekelezaji wa sera ya fedha kwa uwazi. Maamuzi ya Kamati ya Sera ya Fedha ikiwemo kuhusu riba ya Benki Kuu huwasilishwa kwenye mkutano wa Gavana na wakuu wa taasisi za kibenki na pia kwa umma kupitia vyombo vya habari. Vilevile, Benki Kuu huandaa na kuchapisha Tamko la Kamati ya Sera ya Fedha na taarifa mbalimbali zinazoainisha mwelekeo wa sera ya fedha, matokeo ya utekelezaji wake na mwenendo wa uchumi kwa ujumla. Taarifa hizo zinapatikana kwenye tovuti ya Benki Kuu.

**Utekelezaji wa Sera ya Fedha**

i. Mwanzo wa kila mwaka wa fedha, Benki Kuu ya Tanzania hutoa mwelekeo wa sera ya fedha katika Tamko lake la Sera ya Fedha kuendana na malengo ya sera za kiuchumi ya Serikali.

ii. Tamko la Sera ya Fedha huidhinishwa na Bodi ya Wakurugenzi ya Benki Kuu ya Tanzania na kuwasilishwa bungeni kupitia kwa Waziri anayesimamia masuala ya fedha, kama ilivyobainishwa katika kifungu namba 21(5) cha Sheria ya Benki Kuu.

iii. Utaratibu huo pia unafuatwa wakati ya uandaaji wa Mapitio ya nusu mwaka ya Tamko la Sera ya Fedha, ambayo huainisha maendeleo ya utekelezaji wa sera ya fedha dhidi ya malengo yake, matarajio kwa kipindi cha mwaka kilichosalia, na hatua zitakazochukuliwa ili kufikia malengo ya sera.

iv. Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) ya Bodi ya Wakurugenzi ya Benki Kuu, ambayo inaongozwa na Gavana, inawajibika kuamua Riba ya Benki Kuu (CBR) kila robo mwaka, kuendana na malengo ya sera za kiuchumi za Serikali.

v. Kamati ya Ufuatiliaji na Uangalizi ya Menejimenti ya Benki Kuu inakutana kila siku za kazi kutathmini mwenendo wa riba ya mikopo ya siku 7 baina ya benki (kiashiria cha uendeshaji) na kuamua hatua zitakazochukuliwa ili kuhakikisha riba hiyo inabaki ndani ya wigo unaotakiwa.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MALENGO NA UTEKELEZAJI WA SERA YA FEDHA KWA MWAKA 2024/25

### 2.1 Malengo ya Sera ya Fedha

Kwa mwaka 2024/25, sera ya fedha ililenga kuhakikisha kuwa matarajio ya mfumuko wa bei yanabaki ndani ya lengo la asilimia 3 - 5, kuchagiza ukuaji wa uchumi kwa asilimia 5.4 mwaka 2024 kwa Tanzania bara na asilimia 7.2 kwa Zanzibar, na kuhakikisha utulivu wa sekta ya fedha. Kufikia malengo hayo, Benki Kuu ilipanga kutekeleza sera ya fedha kwa kutumia mfumo unaotumia riba ya Benki Kuu (CBR), ulioanza kutumika rasmi mwezi Januari 2024. Kwa muktadha huu, Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) ilikutana kila robo mwaka na kuamua riba ya Benki Kuu, huku utekelezaji wa sera ya fedha ukilenga kuhakikisha riba ya mikopo ya siku saba baina ya benki inabaki ndani ya wigo wa asilimia +/- 2 wa riba ya Benki Kuu

### 2.2 Utekelezaji wa Sera ya Fedha


Utekelezaji wa sera ya fedha kwa mwaka 2024/25 ulikuwa wa kuridhisha na hivyo kuwezesha kufikiwa kwa malengo ya uchumi. Riba ya Benki Kuu ilibaki kuwa asilimia 6, katika robo zote nne za mwaka 2024/25, ili kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei na kuchagiza ukuaji endelevu wa uchumi. Kiwango cha ukwasi kiliwiana na mahitaji ya shughuli za kiuchumi na hivyo kuchochea ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi. Katika kipindi hiki, mfumuko wa bei na ukuaji wa uchumi viliendana na maoteo kwa kiwango kikubwa, huku tofauti iliyoonekana katika baadhi ya robo mwaka ikiwa ndani ya viwango vinavyokubalika.

Riba ya mikopo ya siku saba katika soko la fedha baina ya benki ilikuwa tulivu na ndani ya wigo, ingawa iliongezeka kidogo na kuvuka ukomo wa juu wa CBR katika miezi ya Agosti, Septemba na Oktoba 2024. Kuongezeka kwa riba katika kipindi hicho kulitokana na ongezeko la mahitaji ya fedha kwa ajili ya kununua mazao kufuatia kiasi kikubwa cha mavuno kuliko matarajio, benki za biashara kuongeza uwekezaji kwenye rasilimali zilizo katika fedha za kigeni, na ongezeko la uwekezaji wa wananchi katika dhamana za Serikali, na hivyo kupunguza amana zao katika benki za biashara. Ili kuhakikisha kuwa riba hiyo inabaki ndani ya wigo wa CBR, Benki Kuu iliongeza ukwasi kwa kutumia nyenzo za sera ya fedha, ikiwemo utoaji wa mikopo ya muda mfupi kwa benki za biashara *(reverse repurchase agreements)*, kununua fedha za kigeni katika soko la jumla la fedha za kigeni na kubadilishana fedha za kigeni kwa shilingi na benki (*foreign exchange swap*). Vilevile, Benki Kuu iliongeza ukwasi kupitia programu ya ununuzi wa dhahabu katika soko la ndani[1]. Kufuatia hatua hizi, ukwasi katika benki uliongezeka na riba ya mikopo ya siku saba baina ya benki ilipungua na kuwa ndani ya wigo wa CBR. Vilevile, amana za benki zilizopo Benki Kuu *(clearing balances)* ziliongezeka (Kielelezo 2.1a). Hata hivyo, baadhi ya benki ndogo ziliendelea kukumbwa na changamoto ya kupata ukwasi kwa gharama nafuu kutoka kwa benki kubwa, hali iliyochangia kiwango hicho cha riba kubaki karibu na wigo wa juu wa CBR (Kielelezo 2.1b)

1 Benki Kuu ilianzisha Programu ya Ununuzi wa Dhahabu katika soko la ndani mnamo Septemba 2023, kama moja ya nyenzo za kuongeza akiba ya fedha za kigeni

Utekelezaji wa sera ya fedha, pia uliiwezesha Benki Kuu kufikia malengo yaliyoainishwa katika Programu ya Extended Credit Facility (ECF), chini ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF)[2]. Kufikiwa kwa malengo haya pamoja na maboresho mengine yaliyofanyika chini ya programu hii, kuliwezesha kuidhinishwa kwa fedha za kusaidia bajeti mwezi Januari 2025.


**Kilelezo 2.1a: Amana za Benki na Riba za Mikopo Baina ya Benki**




*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania

2 Extended Credit Facility (ECF) ni programu ya IMF yenye lengo la kutoa msaada wa kifedha ndani ya kipindi cha kati kwa nchi wanachama. Programu hii inalenga kusaidia nchi wanachama kufanya maboresho mbalimbali ili kuongeza uthabiti wa uchumi.

## Kielelezo 2.1b: Riba ya Benki Kuu na Riba ya Mikopo ya Siku 7




*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MWENENDO WA UCHUMI WA DUNIA

### 3.1 Ukuaji wa Uchumi wa Dunia

Uchumi wa dunia uliimarika katika nusu ya pili ya mwaka 2024 kufuatia utekelezaji wa sera ya fedha iliyolenga kuongeza ukwasi kwenye uchumi, hatua za kuchagiza shughuli za kiuchumi zilizochukuliwa na serikali pamoja na ongezeko la matumizi ya walaji. Kufuatia mwenendo huu, Shirika la Fedha Duniani (IMF) linakadiria uchumi wa dunia ulikua kwa asilimia 3.3 mwaka 2024, ukilinganisha na asilimia 3.5 mwaka 2023. Takwimu za ukuaji wa uchumi wa dunia kwa nusu ya kwanza ya mwaka 2025 bado hazichapishwa. Hata hivyo, Nchi zilizoendelea hususan Marekani, ukuaji wa uchumi ulipungua katika robo ya kwanza ya mwaka 2025, kutokana na kutokutabirika kwa sera za biashara na kupungua kwa mahitaji ya walaji. Katika nchi za Umoja wa Ulaya, takwimu za awali zinaonesha dalili ya uchumi kuimarika japo kwa kasi ndogo (Jedwali 3.1).

Kasi ya ukuaji wa uchumi katika nchi za BRICS[3] iliendelea kutofautiana baina ya nchi (Jedwali 3.2). Ukuaji wa uchumi nchini China, Urusi, Afrika Kusini na Brazili ulipungua kutokana na mivutano ya kibiashara inayoendelea, huku ukuaji nchini India ukiongezeka kutokana na ongezeko la mahitaji ya walaji, na uwekezaji unaoendelea katika ujenzi wa miundombinu na sekta ya kidijitali.

3 Brazil, Urusi, India,China na Afrika Kusini.

### Jedwali.3.1: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Nchi zilizoendelea

*Asilimia*

| | 2024 | | | | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| | Robo ya 1 | Robo ya 2 | Robo ya 3 | Robo ya 4 | Robo ya 1 |
| Marekani | 2.9 | 3.0 | 2.7 | 2.5 | 2.0 |
| Eneo la Ulaya | 0.3 | 0.2 | 0.4 | 0.2 | 0.3 |
| Japani | -0.6 | -0.6 | 0.8 | 1.3 | 1.7 |
| Ujerumani | 0.2 | -0.3 | 0.1 | -0.2 | 0.2 |
| Uingereza | 0.7 | 0.5 | 0.0 | 0.1 | 0.7 |

*Chanzo*: Bloomberg

### Jedwali 3.2: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Nchi za BRICS

*Asilimia*

| | 2024 | | | | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| | Robo ya 1 | Robo ya 2 | Robo ya 3 | Robo ya 4 | Robo ya 1 |
| Urusi | n.a | 4.3 | 3.3 | 4.5 | 1.4 |
| India | 8.4 | 6.5 | 5.6 | 6.2 | 6.7 |
| China | 1.5 | 1.0 | 1.4 | 1.6 | 1.2 |
| Afrika Kusini | 0.1 | 0.3 | -0.1 | 0.6 | 0.3 |
| Brazili | 1 | 1.3 | 0.7 | 0.2 | 0.1 |


*Chanzo*: Bloomberg

## 3.2 Mwenendo wa Mfumuko wa Bei

Mfumuko wa bei duniani uliendelea kupungua, japo kwa kasi tofauti baina ya kanda. Hali hii imepelekea kupunguzwa kwa riba za sera ya fedha ili kuchagiza ukuaji wa uchumi. Kwa nchi zilizoendelea, hususan Marekani na Umoja wa Ulaya, mfumuko wa bei uliendelea kupungua kutokana na matokeo ya kubanwa kwa sera ya fedha na kupungua kwa bei za nishati. Nchi zinazoibuka na zinazoendelea kiuchumi, hususan India, mfumuko wa bei umeendelea kushuka kutokana na bei za chakula kupungua kwa kasi zaidi ya ilivyotarajiwa. Aidha, China imeendelea kukabiliana na mfumuko wa bei hasi kutokana na kupungua kwa mahitaji na vikwazo vya kibiashara vilivyowekwa na Marekani. Nchini Afrika Kusini, mfumuko wa bei ulipungua kutokana na kushuka kwa bei za bidhaa katika soko la dunia, pamoja na kuongezeka kwa upatikaji wa chakula (Kielelezo 3.1).

**Kielelezo 3.1: Mfumuko wa bei kwa nchi zilizoendelea na zinazoibukia**

*Asilimia*





*Chanzo*: OECD na Ofisi za Takwimu za Nchi husika

## 3.3 Mwenendo wa Bei za Bidhaa Katika Soko la Dunia

Kwa kipindi cha Julai 2024 - Aprili 2025, bei za bidhaa katika soko la dunia zilikuwa na mwenendo uliotofautiana, ambapo bei za dhahabu, kahawa, mbolea na tumbaku ziliongezeka, huku zile za mafuta ghafi, pamba na sukari zikipungua. Kupanda kwa bei za dhahabu kulitokana na mvutano wa kibiashara unaondelea, na hivyo kusababisha ongezeko la mahitaji ya dhahabu kama rasilimali salama (safe haven) ya uwekezaji na akiba. Bei ya kahawa (Arabica na Robusta) iliongezeka kutokana na matarajio ya kupungua kwa uzalishaji duniani, kufuatia hali mbaya ya hewa hususan kuongezeka kwa joto na mvua za chini ya wastani katika nchi zinazoongoza kwa uzalishaji kama Brazili na Vietnam. Aidha, ongezeko la ushuru kwa malighafi lilipelekea kupanda kwa bei ya mbolea. Kushuka kwa wastani wa bei za mafuta ghafi kulisababishwa kwa kiasi kikubwa na kupungua kwa mahitaji


kutokana na athari za ongezeko kubwa la ushuru wa forodha. Bei ya pamba ilishuka kutokana na kupungua kwa mahitaji duniani, wakati bei za sukari zilipungua kutokana na ongezeko la uzalishaji (Kielelezo 3.2a and 3.2b).

**Kielelezo 3.2a: Bei za Bidhaa katika Soko la Dunia**




*Chanzo* : http://www.worldbank.org/prospects

## Kielelezo 3.2b: Bei za Bidhaa katika Soko la Dunia




*Chanzo*: http://www.worldbank.org/prospects

## 3.4 Mwenendo wa Masoko ya Fedha Duniani

Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, masoko ya fedha duniani yaliathiriwa na mabadiliko ya sera ya fedha, na kutotabirika kwa hali za kisiasa duniani. Nchini Marekani, riba za hati fungani za serikali

ziliendelea kuwa juu, ambapo riba ya hatifungani ya miaka 10 ilikuwa kati ya asilimia 4.1 na 4.6. Kwa muktadha huu, Benki Kuu nchini Marekani iliendelea kuchukua tahadhari katika kupunguza viwango vya riba ya sera ya fedha, kutokana na mfumuko wa bei wa msingi (*core inflation*) kubaki juu ya asilimia 3 sambamba na ongezeko la bei katika sekta za makazi na huduma. Riba za hati fungani za serikali ziliendelea kuwa na mabadiliko makubwa katika nchi za Umoja wa Ulaya. Licha ya mwenendo mzuri wa mfumuko wa bei, Benki Kuu ya Ulaya imeendelea kuchukua tahadhari, huku ikibainisha kuwa maamuzi ya kushusha riba ya sera ya fedha yatafanyika taratibu, kwa kuzingatia zaidi mwenendo wa ukuaji wa uchumi.

Nchini China, riba za hati fungani za serikali ziliendelea kuwa chini, ambapo riba ya hati fungani ya miaka 10 ilibaki kati ya asilimia 2.3 hadi asilimia 2.6. Benki Kuu ya China iliendelea kutekeleza sera ya fedha inayolenga kuongeza ukwasi kwenye uchumi kufuatia kupungua kwa mahitaji ya ndani na mfumuko wa bei.

Kuelekea Juni 2025, masoko ya fedha yanatarajiwa kuendelea kuathiriwa na taarifa za kiuchumi pamoja na maamuzi ya kisera, hususan katika benki kuu za nchi zilizoendelea. Aidha, kufuatia kupungua kwa mfumuko wa bei na kasi ya ukuaji wa uchumi, benki kuu katika baadhi ya nchi zilizoendelea zinatarajiwa kuendelea kupunguza viwango vya riba za sera ya fedha. Hata hivyo, hali ya kutokutabirika kwa sera za kibiashara na migogoro ya kisiasa inayoendelea, vinaweza kuathiri utulivu wa masoko ya fedha. Kwa mantiki hii, kuna haja ya kuhakikisha uwepo wa akiba ya kutosha ya fedha za kigeni, na kuendelea kufuatilia kwa umakini mwenendo wa sarafu mbalimbali, na kufanya maamuzi sahihi katika uwekezaji na utekelezaji wa sera za fedha kuendana na mwenendo wa masoko ya fedha duniani.


# SEHEMU YA NNE

## 4.0 MWENENDO WA UCHUMI NCHINI

### 4.1 Pato la Taifa

Mwenendo wa ukuaji wa uchumi nchini ulikua imara kwa mwaka 2024, ukichangiwa zaidi na uwekezaji unaoendelea kufanywa na Serikali na sekta binafsi. Kwa upande wa Tanzania Bara, uchumi ulikua kwa asilimia 5.5, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.1 mwaka 2023 na makadirio ya ukuaji wa asilimia 5.4 (Kielelezo 4.1a). Ukuaji huu ulichangiwa zaidi na shughuli za kilimo, ujenzi, fedha na bima, pamoja na shughuli za uchimbaji madini na mawe (Kielelezo 4.1b). Ukuaji huo pia ulichangiwa na utekelezaji wa mipango mbalimbali ya Serikali ikiwemo matumizi ya pembejeo bora za kilimo, upatikanaji wa umeme wa uhakika, utekelezaji wa miradi ya miundombinu, utekelezaji wa mipango ya huduma jumuishi za fedha, na uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji. Aidha, bei nzuri za bidhaa katika soko la dunia kama vile dhahabu, korosho, na kahawa pia zilichangia katika kuimarika kwa uchumi.


**Kielelezo 4.1a: Ukuaji wa Pato la Taifa**




*Chanzo:* Ofisi ya Taifa ya Takwimu

**Kielelezo 4.1b: Mchango wa Baadhi ya Shughuli za Uchumi katika Ukuaji wa Pato la Taifa**

*Asilimia*





*Chanzo:* Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Uchumi wa Zanzibar ulikua kwa asilimia 7.1 mwaka 2024, chini kidogo ya ukuaji wa asilimia 7.4 mwaka 2023 na makadirio ya ukuaji wa asilimia 7.2, kufuatia kukamilika kwa baadhi ya miradi mikubwa ya miundombinu na uwekezaji (Kielelezo 4.2a na 4.2b). Licha ya mwenendo huu, uchumi uliendelea kuwa imara ukichangiwa zaidi na shughuli za malazi na huduma za chakula, kufuatia ongezeko la idadi ya watalii kufikia 736,755 mwaka 2024 kutoka 638,498 mwaka 2023.

## Kielelezo 4.2a: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Zanzibar


*Asilimia*




*Chanzo:* Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar

## Kielelezo 4.2b: Mchango wa Baadhi ya Shughuli za Uchumi katika Ukuaji wa Pato la Taifa

*Asilimia*





*Chanzo:* Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar

## 4.2 Mfumuko wa Bei


Mfumuko wa bei umeendelea kuwa chini na tulivu ndani ya lengo la nchi na vigezo vya mtangamano wa kiuchumi kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Umoja wa Maendeleo wa Kusini mwa Afrika (SADC) . Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, mfumuko wa bei kwa Tanzania bara ulikuwa wastani wa asilimia 3.1 (Kielelezo 4.3a na 43b). Matokeo haya yalichangiwa zaidi na utekelezaji madhubuti wa sera ya fedha pamoja na kupungua kwa bei za bidhaa zisizo za chakula. Mwenendo wa mfumuko wa bei wa jumla *(overall inflation)* kwa Tanzania Bara uliendelea kuchangiwa zaidi na mfumuko wa bei wa msingi *(core inflation)* na wa chakula (Kielelezo 4.3c). Mchango wa mfumuko wa bei wa msingi kwa mfumuko wa bei wa jumla uliendelea kuwa wa juu licha ya kushuka hadi asilimia 1.7 mwezi Machi na Aprili 2025. Mfumuko wa bei za chakula uliongezeka kidogo hadi wastani wa asilimia 3.8, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24, hivyo kusababisha mchango wake kwenye mfumuko wa bei wa jumla kuongezeka. Hali hii ilichangiwa zaidi na kupanda kwa bei za ulezi, viazi mviringo, mtama, na maharagwe. Mfumuko wa bei katika ukanda wa EAC na SADC ulitofautiana baina ya nchi, huku nchi nyingi zikifikia vigezo vya mtangamano (Kielelezo 4.3d na 4.3e).

## Kielelezo 4.3a: Mfumuko wa Bei





*Chanzo:* Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## Kielelezo 4.3b: Mfumuko wa Bei na Malengo ya Nchi na Kikanda




*Chanzo:* Ofisi ya Taifa ya Takwimu


## Kielelezo 4.3c: Mchango katika Mfumuko wa Bei




*Chanzo:* Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## Kielelezo 4.3d: Mfumuko wa Bei kwa Nchi za EAC


*Asilimia*




*Chanzo*: Ofisi za Takwimu za Nchi husika
*Tanbihi*: Mistari nukta inamaanisha kigezo cha mtangamano kwa nchi za EAC cha asilimia 8

## Kielelezo 4.3e: Mfumuko wa Bei kwa Nchi za SADC


*Asilimia*




*Chanzo*: Ofisi za Takwimu za Nchi husika
Tanbihi: Mistari nukta inamaanisha kigezo cha mtangamano kwa nchi za SADC cha asilimia 3-7

Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, mfumuko wa bei kwa Zanzibar ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 5, kutoka asilimia 5.9 iliyorekodiwa katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Mwenendo huu ulichangiwa zaidi na kupungua kwa bei za chakula (Kielelezo 4.4). Mfumuko wa bei za chakula ulipungua hadi wastani wa asilimia 7.1 kutoka asilimia 10.4 katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024, kunatokana na upatikanaji wa chakula wa kutosha nchini. Mfumuko wa bei wa bidhaa zisizo za chakula uliongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 3.4 kutoka asilimia 2.9 iliyorekodiwa katika kipindi kama hicho mwaka uliopita, ukichangiwa zaidi na kupanda kwa bei mafuta ya petroli na dizeli.

**Kielelelezo 4.4: Mfumuko wa Bei kwa Zanzibar**





*Chanzo*: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar

## 4.3 Mwenendo wa Ujazi wa Fedha na Mikopo kwa Sekta Binafsi


Ujazi wa fedha uliendelea kukua kwa kasi ya kuridhisha katika miezi kumi ya mwanzo ya mwaka 2024/25. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa wastani wa asilimia 13.8, ikilinganishwa na asilimia 14.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Ukuaji huu umechangiwa zaidi na mikopo kwa sekta binafsi (Kielelezo 4.5a na 4.5b).

## Kielelezo 4.5a: Ukuaji wa Ujazi wa Fedha na Mikopo kwa Sekta Binafsi




*Chanzo*: Benki Kuu ya Tanzania


## Kielelezo 4.5b: Mchango wa Ukuaji wa M3




*Chanzo*: Benki Kuu ya Tanzania


Mikopo kwa sekta binafsi ilikua kwa wastani wa asilimia 15.1 katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 18.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi kunaakisi utekelezaji wa sera ya fedha iliyolenga kudhibiti viashiria vya mfumuko wa bei kutokana na kupungua kwa thamani ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni. Uwiano wa mikopo kwa sekta binafsi dhidi ya Pato la Taifa, ambao ni kiashiria cha ukuaji wa sekta ya fedha, ulikuwa kwa asilimia 19.5 ikilinganishwa na asilimia 16.9, kutokana na kuimarika kwa mazingira ya biashara, utekekezaji wa sera madhubuti za fedha na bajeti na kuendelea kuimarika kwa shughuli za kiuchumi nchini. Mikopo inayoelekezwa kwa shughuli binafsi za uzalishaji, iliendelea kuchukua sehemu kubwa ya mikopo yote, huku ikichangia zaidi katika ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi (Kielelezo 4.6a na Kielelezo 4.6b). Mikopo kwa sekta ya kilimo imeendelea kuongezeka ikiwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 40 huku mchango wake katika mikopo yote ukiongezeka hadi asilimia 24, kutoka asilimia 18 katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Mwenendo huu umechangiwa kwa kiwango kikubwa na mikopo inayotolewa kwa benki na taasisi za fedha kupitia mkopo maalumu wa Shilingi Trilioni 1, na unafuu unaotolewa kwa kiwango cha amana zinazotakiwa kuwekwa kisheria Benki Kuu, pale benki zinapotoa mikopo kwa sekta ya kilimo kwa riba isiyozidi asilimia 10. Vilevile, juhudi za serikali za kuongeza tija na uzalishaji katika sekta ya kilimo kupitia utoaji wa fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya umwagiliaji, huduma za ugani, na tafiti, zimehamasisha benki kuongeza mikopo kwa sekta hiyo. Vilevile, utoaji wa ruzuku kwa mbolea na mbegu, umechochea uzalishaji katika sekta ya kilimo.

## Kielelezo 4.6a: Mchango wa Shughuli za kiuchumi katika Ukuaji wa Mikopo, kwa Asilimia




*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania

## Kielelezo 4.6b: Mgawanyo wa Mikopo kwa Shughuli za Kiuchumi, kwa Asilimia





*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania

## 4.4 Viwango vya Riba

Kwa kipindi cha miezi kumi ya mwanzo ya mwaka 2024/25, riba za mikopo hazikuwa na mabadiliko makubwa ikilinganishwa na viwango vilivyorekodiwa kipindi kama hicho mwaka 2023/24, zikiwa na wastani wa asilimia 15.5. Aidha, riba za amana ziliongezeka kwa kiasi kidogo hadi asilimia 8.14 kutoka asilimia 7 (Kielelezo 4.7a). Riba za mikopo kwa wateja wakubwa (*negotiated lending rates*) zilibakia kuwa takriban asilimia 13, huku viwango vya riba za amana kwa wateja wakubwa vikiongezeka hadi asilimia 10.48, kutoka asilimia 9.30 (Kielelezo 4.7a). Riba za dhamana za serikali (*Treasury bills*) ziliongezeka katika nusu ya kwanza ya mwaka 2024/25, japokuwa zilianza kupungua mwanzoni mwa nusu ya pili ya mwaka 2024/25 sambamba na mwenendo wa ukwasi katika benki (Kielelezo 4.7b).


Riba za mikopo zimeendelea kushuka kwa kasi ndogo, hali inayoashiria uwepo kwa changamoto za kimuundo katika upangaji wa riba za mikopo. Serikali na Benki Kuu zinaendelea kufanya maboresho katika kukabiliana na changamoto hizo zinazoathiri pia ufanisi wa sera ya fedha. Hatua hizo ni pamoja na kufuatilia uzingatiaji wa Kanuni za Kumlinda Mteja wa Huduma za Kifedha za mwaka (2019); kuboresha upatikanaji wa taarifa za wateja kupitia utoaji wa vitambulisho vya taifa na urasmishaji wa anuani za makazi; na kutekeleza maboresho katika mfumo wa mahakama ili kuharakisha utatuzi wa migogoro inayohusiana na mikopo. Vilevile, Benki ya Tanzania inakamilisha uundaji wa Mfumo wa Kulinganisha Bei (*Price Comparator System*) utakaowawezesha wateja kufanya tathmini ya viwango vya bei na tozo za huduma mbalimbali za fedha katika benki tofauti, ili waweze kufanya maamuzi sahihi.

## Kielelezo 4.7a: Riba za Amana na Mikopo Inayotolewa Benki za Biashara




*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania

## Kielelezo 4.7b: Riba katika Masoko ya Fedha




*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania

## 4.5 Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali

Kwa miezi kumi ya mwaka 2024/25, utekelezaji wa bajeti ya Serikali ulikuwa wa kuridhisha huku matumizi yakiendana na rasilimali zilizopo. Kwa upande wa Tanzania Bara mapato ya kodi na yasiyo ya kodi yalikuwa shilingi bilioni 27,830.7 sawa na asilimia 99 ya makadirio (Jedwali 4.2). Ufanisi huu ulitokana kwa kiwango kikubwa na makusanyo ya kodi ambayo yalifikia asilimia 102.2 ya lengo, kufuatia ongezeko la ulipaji kodi kwa hiyari kutokana na jitihada zinazoendelea kufanywa na Serikali kuelimisha wananchi juu ya umuhimu wa kulipa kodi pamoja na kuimarika kwa usimamizi katika ukusanyaji wa kodi na shughuli za kiuchumi. Wakati huohuo, matumizi ya Serikali yalikuwa Shilingi 34,149, ambapo matumizi kwa ajili ya kugharamia shughuli za maendeleo yalikuwa ni asilimia 33.5, sanjari na jitihada za Serikali katika kuboresha miundombinu na mikakati ya kuchochea ukuaji wa uchumi (Jedwali 4.1).

**Jedwali 4.1: Muhtasari wa Utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa Tanzania Bara**

*Shilingi Bilioni*

| | Julai-23 - Aprili-24 | Julai-24 - Aprili-25 | | |
|---|---|---|---|---|
| | Halisi | Makadirio | Halisi | Halisi/Makadirio (%) |
| Mapato | 24,148.2 | 28,125.4 | 27,830.7 | 99.0 |
| Matumizi | 29,544.7 | 35,511.0 | 34,149.0 | 96.2 |
| Matumizi ya kawaida | 17,401.8 | 22,709.1 | 22,719.1 | 100.0 |
| Matumizi ya maendeleo | 12,142.9 | 12,801.9 | 11,429.9 | 89.3 |


*Source*: Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania

Kwa upande wa Zanzibar, mapato ya Serikali, yakijumuisha mapato ya ndani na misaada kutoka nje, yaliongezeka na kufikia shilingi bilioni 1,571.3 kwa kipindi cha mwezi Julai hadi Aprili 2024/25, ikiwa ni juu

ya lengo kwa asilimia 1.5. Mapato ya ndani yalikuwa shilingi bilioni 1,443.0, sawa na asimilia 99.2 ya lengo, wakati misaada kutoka kwa wadau wa maendeleo ilikuwa ni shilingi bilioni 128.3, yakivuka lengo kwa asilimia 35.6. Mapato ya kodi, yalifikia shillingi bilioni 1,268.6, juu ya lengo kwa asilimia 3.0 na mapato yasiyo ya kodi yalifikia shilingi bilioni 174.4, sawa na asilimia 78.5 ya lengo (Kielelezo 4.8a). Aidha, ukusanyaji wa mapato ulivuka malengo katika makundi yote ya kodi kutokana na kuongezeka kwa ufanisi katika usimamizi na ukusanyaji kodi na pamoja na utayari wa walipakodi kulipa kodi kwa hiyari. Matumizi ya serikali yalikuwa shillingi bilioni 2,255.2, ambapo matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi bilion 1,209.6 na matumizi kwa ajili ya miradi ya maendeleo yalikua shilingi bilioni 1,045.6 (Kielelezo 4.8b).

**Kielelezo 4.8a: Mapato ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar**


*Shilingi Bilioni*




*Chanzo*: Wizara ya Fedha na Mipango, Zanzibar

**Kielelezo 4.8b: Matumizi ya Serikali ya Mapinduzi Zanzibar**

*Shilingi Bilioni*




*Chanzo*: Wizara ya Fedha na Mipango, Zanzibar

## 4.6 Deni la Taifa

Deni la Serikali Kuu linalojumuisha deni la ndani na nje lilifikia dola za Marekani milioni 40,201.7, mwishoni mwa mwezi Aprili 2025 ikiwa ni ongezeko la asilimia 9.5 kutoka kiwango kilichorekodiwa mwezi Juni 2024 (Jedwali 4.2a). Ongezeko hili lilitokana na mikopo mipya iliyochukuliwa kwa ajili ya kugharamia miradi na shughuli za maendeleo.

Deni la nje liliongezeka kwa asilimia 10.8 kutoka kiwango kilichorekodiwa mwishoni mwa Juni 2024, likiwa sawa na asilimia 67.7 ya deni la Serikali Kuu. Sehemu kubwa ya deni la nje la Serikali Kuu ilikuwa ni mikopo yenye masharti nafuu kutoka taasisi za kimataifa, ikifuatiwa na mikopo ya kibiashara (Jedwali 4.2b). Sehemu kubwa ya fedha zilizotokana na mikopo ya nje ilielekezwa kwenye miradi ya maendeleo katika sekta za usafirishaji na mawasiliano (Jedwali 4.2c). Hadi kufikia mwishoni mwa mwezi Aprili 2025, deni la ndani la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 34,759.9, ikiwa ni ongezeko la asilimia 8.8 kutoka mwezi Juni 2024. Ongezeko hili kwa kiasi kikubwa lilichangiwa na mauzo ya dhamana za Serikali za muda mrefu ambazo ziliongezeka kwa shilingi bilioni 2,708.6, ikiwa pia ni

sehemu kubwa ya deni la ndani la Serikali (Jedwali 4.2d). Deni la ndani la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar lilifikia shilingi bilioni 1,313.2 mwishoni mwa Aprili 2025, ambapo kiasi kikubwa kilikuwa ni dhamana za Serikali ikifuatiwa na mikopo kutoka benki za biashara.

## Jedwali 4.2a: Deni la Taifa

*Dola milioni*

| | Des-23 | Jun-24 | Des-24 | Apr-25[a] |
|---|---|---|---|---|
| Deni la Serikali kuu | 35,574.0 | 36,732.4 | 39,510.7 | 40,201.7 |
| Deni la nje | 23,422.0 | 24,569.4 | 25,877.1 | 27,227.8 |
| % ya deni la Serikali | 65.8 | 66.9 | 65.5 | 67.7 |
| Deni la ndani | 12,152.0 | 12,163.0 | 13,633.7 | 12,974.0 |
| Deni la nje la sekta binafsi | 6,954.5 | 7,377.7 | 8,149.7 | 8,278.1 |
| Deni la nje la mashirika ya umma | 5.0 | 3.8 | 3.8 | 3.8 |
| Jumla ya deni la nje | 30,381.5 | 31,950.9 | 34,030.6 | 35,505.9 |
| Jumla ya deni la Taifa | 42,533.5 | 44,113.8 | 47,664.2 | 48,479.9 |

*Source:* Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
*Tanbihi*: a inamaanisha takwimu za awali

## Jedwali 4.2b: Wadai wa Deni la Nje

*Dola Milioni*

| | Jun-24 | | Des-24 | | Apr-25[a] | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Aina ya wakopeshaji | Kiasi | Asilimia | Kiasi | Asilimia | Kiasi | Asilimia |
| Mashirika ya kimataifa | 17,148.6 | 53.7 | 18,235.0 | 53.6 | 19,051.6 | 53.7 |
| Deni ambalo halijalipwa | 17,052.9 | 53.4 | 18,122.6 | 53.3 | 18,963.8 | 53.4 |
| Malimbikizo ya riba | 95.6 | 0.3 | 112.4 | 0.3 | 87.8 | 0.2 |
| Nchi wahisani | 1,360.2 | 4.3 | 1,270.3 | 3.7 | 1,456.1 | 4.1 |
| Deni ambalo halijalipwa | 1,108.4 | 3.5 | 1,193.2 | 3.5 | 1,378.2 | 3.9 |
| Malimbikizo ya riba | 251.9 | 0.8 | 77.2 | 0.2 | 78.0 | 0.2 |
| Kibiashara | 11,742.1 | 36.8 | 12,606.6 | 37.0 | 13,088.5 | 36.9 |
| Deni ambalo halijalipwa | 10,944.2 | 34.3 | 11,583.5 | 34.0 | 12,043.5 | 33.9 |
| Malimbikizo ya riba | 797.9 | 2.5 | 1,023.1 | 3.0 | 1,045.0 | 2.9 |
| Mkopo wa kuuza nje | 1,700.0 | 5.3 | 1,918.7 | 5.6 | 1,909.7 | 5.4 |
| Deni ambalo halijalipwa | 1,310.5 | 4.1 | 1,424.5 | 4.2 | 1,405.5 | 4.0 |
| Malimbikizo ya riba | 389.5 | 1.2 | 494.1 | 1.5 | 504.2 | 1.4 |
| Deni la nje | 31,950.9 | 100.0 | 34,030.6 | 100.0 | 35,505.9 | 100.0 |

*Source:* Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
*Tanbihi*: a inamaanisha takwimu za awali

## Jedwali 4.2c Matumizi ya Mikopo ya Nje Iliyopokelewa

*Dola Milioni*

| | Jun-24 | | Des-24 | | Apr-25[a] | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Shughuli ya kiuchumi | Kiasi | Asilimia | Kiasi | Asilimia | Kiasi | Asilimia |
| Urari wa malipo na msaada wa kibajeti | 5,358.1 | 17.6 | 6,396.2 | 19.8 | 6,832.9 | 20.2 |
| Usafirishaji na mawasiliano | 6,470.5 | 21.3 | 6,726.2 | 20.8 | 7,272.0 | 21.5 |
| Kilimo | 1,561.1 | 5.1 | 1,627.0 | 5.0 | 1,711.3 | 5.1 |
| Nishati na madini | 4,625.1 | 15.2 | 4,615.6 | 14.3 | 4,591.5 | 13.6 |
| Viwanda | 1,224.0 | 4.0 | 1,281.8 | 4.0 | 1,331.0 | 3.9 |
| Huduma za jamii na elimu | 6,181.3 | 20.3 | 6,386.0 | 19.8 | 6,736.4 | 19.9 |
| Fedha na bima | 1,197.2 | 3.9 | 1,337.6 | 4.1 | 1,332.7 | 3.9 |
| Utalii | 508.4 | 1.7 | 515.9 | 1.6 | 551.7 | 1.6 |
| Mali isiyohamishika na ujenzi | 1,521.5 | 5.0 | 1,608.0 | 5.0 | 1,601.2 | 4.7 |
| Mengineyo | 1,768.8 | 5.8 | 1,829.4 | 5.7 | 1,830.4 | 5.4 |
| Jumla | 30,416.1 | 100.0 | 32,323.8 | 100.0 | 33,790.9 | 100.0 |

*Chanzo:* Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
*Tanbihi:* a, inamaanisha takwimu za awali

## Jedwali 4.2d: Deni la Ndani

*Shilingi Bilioni*

| | Jun-24 | | Des-24 | | Apr-25[a] | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Nyenzo | Kiasi | Asilimia | Kiasi | Asilimia | Kiasi | Asilimia |
| Dhamana za serikali | 27,266.8 | 85.3 | 28,664.3 | 87.8 | 29,582.4 | 85.1 |
| Dhamana za serikali za muda mfupi | 2,328.7 | 7.3 | 2,108.0 | 6.5 | 1,935.6 | 5.6 |
| Hisa za serikali | 187.1 | 0.6 | 187.1 | 0.6 | 187.1 | 0.5 |
| Dhamana za serikali za muda mrefu | 24,751.0 | 77.5 | 26,369.1 | 80.8 | 27,459.6 | 79.0 |
| Vyeti vya ushuru | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.0 | 0.1 | 0.0 |
| Deni lisilo na dhamana | 4,684.5 | 14.7 | 3,985.0 | 12.2 | 5,177.5 | 14.9 |
| Madeni mengine* | 18.4 | 0.1 | 18.4 | 0.1 | 18.4 | 0.1 |
| Bakaa hasi | 4,666.1 | 14.6 | 3,966.6 | 12.1 | 5,159.1 | 14.8 |
| Deni la ndani (ukiondoa karatasi za ukwasi) | 31,951.2 | 100.0 | 32,649.3 | 100.0 | 34,759.9 | 100.0 |

*Chanzo:* Wizara ya Fedha na Benki Kuu ya Tanzania
*Tanbihi:* a, inamaanisha takwimu za awali

## 4.7 Mwenendo wa Sekta ya Nje

Sekta ya nje imeendelea kuimarika katika kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, licha ya migogoro ya kisiasa na mvutano wa kibiashara duniani. Nakisi ya urari wa malipo ya kawaida ilipungua hadi dola za Marekani milioni 1,677.3 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni

2,219.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Kuimarika huku kulichangiwa zaidi na ongezeko la mauzo nje ya nchi hususan mapato ya utalii na dhahabu, sambamba na kupungua kwa kasi ya uagizaji wa bidhaa kutoka nje, hususan mafuta ya petroli (Jedwali 4.3). Mwenendo huu unatarajiwa kuendelea katika kipindi cha muda wa kati, sambamba na jitihada za serikali za kuongeza mauzo ya nje na uzalishaji ndani ya nchi wa bidhaa zinazoagizwa kutoka nje. Aidha, kuongezeka kwa bei ya dhahabu na kupungua kwa bei ya mafuta ghafi katika soko la dunia kutachangia kuimarika kwa sekta ya nje. Akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 5,307.7 mwezi Aprili 2025, ikiwa inatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi kwa takriban miezi 4.3 sawia na lengo la nchi la angalau miezi minne (Kielelezo 4.9).


### Jedwali 4.3: Urari wa Malipo ya Kawaida

*Dola Milioni*

| | Mwaka | | | Julai - Aprili | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2022 | 2023 | 2024[a] | 2023/24 | 2024/25[a] |
| Urari wa bidhaa | -6,984.9 | -6,032.3 | -5,157.2 | -4,985.6 | -4,006.4 |
| Zilizouzwa nje* | 7,223.8 | 7,696.6 | 9,121.6 | 6,556.3 | 8,468.0 |
| Zilizonunuliwa nje | -14,208.7 | -13,728.9 | -14,278.9 | -11,541.9 | -12,474.4 |
| Urari wa huduma | 2,296.6 | 3,835.9 | 4,290.5 | 3,604.9 | 3,484.0 |
| Mapato | 4,762.0 | 6,231.7 | 6,899.4 | 5,577.3 | 5,939.4 |
| Malipo | -2,465.4 | -2,395.9 | -2,608.9 | -1,972.4 | -2,455.5 |
| Urari wa Bidhaa na Huduma | -4,688.3 | -2,196.5 | -866.7 | -1,380.7 | -522.4 |
| Bidhaa na Huduma zilizouzwa nje | 11,985.8 | 13,928.3 | 16,021.1 | 12,133.6 | 14,407.4 |
| Bidhaa na Huduma zilizonunuliwa kutoka nje | -16,674.1 | -16,124.8 | -16,887.8 | -13,514.4 | -14,929.9 |
| Urari wa mapato ya vitega uchumi | -1,393.2 | -1,496.6 | -1,742.0 | -1,344.9 | -1,572.5 |
| Yaliyoingia | 183.9 | 301.2 | 356.4 | 275.8 | 335.9 |
| Yaliyotoka | -1,577.1 | -1,797.7 | -2,098.4 | -1,620.7 | -1,908.4 |
| Urari wa uhamisho mali ya kawaida | 599.3 | 732.5 | 576.7 | 505.8 | 417.7 |
| Iliyoingia | 716.5 | 1,280.9 | 1,177.4 | 1,079.5 | 884.1 |
| ambapo Serikalini | 76.4 | 131.0 | 139.2 | 85.7 | 96.2 |
| Iliyoingia | -117.2 | -548.4 | -600.7 | -573.6 | -466.4 |
| Urari wa Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali | -5,482.2 | -2,960.6 | -2,032.0 | -2,219.8 | -1,677.3 |


*Chanzo:* Mamlaka ya Mapato Tanzania Benki Kuu ya Tanzania
*Tanbihi:* a- inamaanisha takwimu za awali
*Zinajumuisha marekebisho kwa ajili ya mauzo nje ya nchi yasiyorekodiwa

### Kielezo 4.9a: Akiba ya Fedha za Kigeni




*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania

### Kielezo 4.9b: Miezi ya Uagizaji wa Bidhaa na Huduma




*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania

Mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yameendelea kuongezeka. Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, mauzo ya bidhaa na huduma yalifikia dola za Marekani milioni 14,407.4, kutoka dola za Marekani milioni 12,133.6 katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na mauzo ya dhahabu, utalii, korosho, tumbaku na mazao ya mbogamboga (Jedwali 4.4 na Kielelezo 4.10). Mauzo ya bidhaa yalifikia dola za Marekani milioni 8,468, yakichangiwa zaidi na dhahabu, ambayo ni sawa na asilimia 39.8 ya mauzo yote ya bidhaa. Mauzo ya huduma yalikuwa dola za Marekani milioni 5,939.4 yakichangiwa zaidi na shughuli za utalii pamoja na huduma za usafirishaji, ambapo kwa pamoja yamechangia asilimia 91 ya mapato yote ya huduma.

### Jedwali 4.4: Mauzo ya Bidhaa na Huduma Nje ya Nchi


*Dola Milioni*

| | Mwaka | | | Julai - Aprili | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2022 | 2023 | 2024[a] | 2023/24 | 2024/25[a] |
| Bidhaa asilia | 766.5 | 953.3 | 1,473.3 | 1,001.3 | 1,500.6 |
| Bidhaa zisizo asilia | 6,058.4 | 6,321.6 | 7,228.8 | 5,218.9 | 6,605.8 |
| ambapo Dhahabu | 2,835.1 | 3,058.9 | 3,419.6 | 2,592.7 | 3,371.7 |
| Bidhaa za viwandani | 1,419.2 | 1,363.3 | 1,341.3 | 1,139.7 | 1,118.8 |
| Mazao ya mboga na maua | 289.6 | 417.2 | 507.1 | 379.2 | 462.4 |
| Mapato ya huduma | 4,762.0 | 6,231.7 | 6,899.4 | 5,577.3 | 5,939.4 |
| ambapo Utalii | 2,527.8 | 3,373.8 | 3,903.1 | 3,117.1 | 3,280.0 |
| Usafirishaji | 1,872.0 | 2,333.4 | 2,356.6 | 1,962.6 | 2,102.9 |
| Mauzo ya bidhaa na huduma | 11,985.8 | 13,928.3 | 16,021.1 | 12,133.6 | 14,407.4 |

*Chanzo:* Mamlaka ya Mapato Tanzania Benki Kuu ya Tanzania
*Tanbihi:* *a* inamaanisha takwimu za awali

## Kielelezo 4.10: Mauzo ya Bidhaa na Huduma Nje ya Nchi

*Dola Milioni*




*Chanzo:* Mamlaka ya Mapato Tanzania Benki Kuu ya Tanzania
*Tanbihi:* *a* inamaanisha takwimu za awali

Uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi uliongezeka, japo kwa kasi ndogo ikilinganishwa na mauzo nje ya nchi. Uagizaji wa bidhaa na huduma ulifikia dola za Marekani milioni 14,929.9 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 13,514.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Uagizaji wa bidhaa, ambao ulichangia asilimia 86 ya uagizaji wote, uliongezeka, ukichangiwa zaidi na malighafi za viwandani, vyombo vya usafiri pamoja na mashine na mitambo, sanjari na dira ya Taifa kuelekea uchumi wa viwanda. Vilevile, malipo kwa ajili ya huduma yaliongezeka na kufikia dola za Marekani milioni 2,455.5 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 1,972.4, huku sehemu kubwa ikiwa ni malipo kwa ajili ya usafirishaji mizigo, sambamba na ongezeko la bidhaa zilizoagizwa toka nje ya nchi. Aidha, uagizaji wa mafuta ya petroli, ambao ulichangia asilimia 17 ya bidhaa zote zilizoagizwa, ulipungua kutokana na kushuka kwa bei ya mafuta ghafi katika soko la dunia (Jedwali 4.5).

## Jedwali 4.5: Bidhaa Zilizoagizwa Kutoka Nje ya Nchi

*Dola Milioni*

| | Mwaka | | | Julai- Aprili | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2022 | 2023 | 2024[a] | 2023/24 | 2024/25[a] |
| Bidhaa za kukuza mtaji | 2,594.0 | 2,893.4 | 3,003.5 | 2,358.1 | 2,801.4 |
| Mashine na mitambo | 1,128.9 | 1,242.7 | 1,092.4 | 920.6 | 1,060.2 |
| Vifaa vya usafiri wa viwandani | 823.2 | 937.2 | 1,136.4 | 810.7 | 1,085.7 |
| Bidhaa za kati | 10,231.0 | 9,389.1 | 9,868.6 | 8,021.7 | 8,381.6 |
| Malighafi za viwanda | 4,780.1 | 4,307.1 | 4,652.8 | 3,701.7 | 4,146.7 |
| Mafuta na vilainishi | 3,482.9 | 2,915.7 | 2,786.1 | 2,536.5 | 2,222.5 |
| ambapo Bidhaa za petroli zilizochujwa | 3,314.8 | 2,725.8 | 2,554.3 | 2,351.2 | 2,124.4 |
| Vifaa | 987.5 | 998.6 | 1,099.6 | 796.0 | 977.5 |
| Chakula na vinywaji kwa matumizi ya viwandani | 717.9 | 828.8 | 953.9 | 721.7 | 698.7 |
| ambapo Ngano | 302.4 | 418.8 | 357.5 | 281.9 | 285.0 |
| Magari binafsi | 257.5 | 338.1 | 374.6 | 265.3 | 334.9 |
| Bidhaa za matumizi ya kawaida | 1,381.5 | 1,444.2 | 1,404.6 | 1,160.3 | 1,288.6 |
| Chakula na vinywaji kwa matumizi ya kawaida | 182.0 | 240.1 | 192.8 | 147.5 | 153.5 |
| Vifaa vya usafiri wa kawaida | 159.5 | 141.7 | 166.3 | 127.1 | 136.4 |
| Bidhaa nyingine za matumizi ya kawaida | 1,040.1 | 1,062.4 | 1,045.5 | 885.6 | 882.0 |
| Malipo ya huduma | 2,465.4 | 2,395.9 | 2,608.9 | 1,972.4 | 2,455.5 |
| O/w Transportation | 342.9 | 1,444.2 | 1,404.6 | 1,082.2 | 1,246.0 |
| Utalii | 142.2 | 240.1 | 192.8 | 317.7 | 470.3 |
| Huduma nyinginezo | 69.9 | 141.7 | 166.3 | 572.5 | 739.2 |
| Bidhaa na huduma | 16,674.1 | 16,124.8 | 16,887.8 | 13,514.2 | 14,929.9 |

*Chanzo:* Mamlaka ya Mapato Tanzania Benki Kuu ya Tanzania
*Tanbihi: a* inamaanisha takwimu za awali
*Zinajumuisha marekebisho kwa ajili ya mauzo nje ya nchi yasiyorekodiwa

Kwa kipindi cha Julai 2024 hadi Aprili 2025, ziada ya urari wa malipo ya kawaida kwa Zanzibar iliongezeka kwa asilimia 46.7 hadi dola za Marekani 719.1 kutoka dola za Marekani 490.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Ongezeko hili lilichangiwa na mapato yatokanayo na shughuli za utalii na kupungua kwa uagizaji wa bidhaa nje ya nchi kwa asilimia 32.1. Aidha uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi ulipungua kwa asilimia 32.3 hadi dola za marekani 437.4 kutokana na kupungua kwa uagizaji wa vyombo vya usafiri na mafuta ya petroli (Jedwali 4.6, Kielelezo 4.11a na 4.11b).

## Jedwali 4.6: Urari wa Malipo ya Kawaida kwa Zanzibar


*Dola Milioni*

| | Julai - Aprili | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25[a] |
| Urari wa bidhaa | -209.4 | -232.5 | -392.9 | -473.0 | -338.7 |
| Zilizouzwa nje | 23.2 | 85.3 | 61.5 | 66.8 | 27.9 |
| Zilizonunuliwa nje | 232.6 | 317.8 | 420.2 | 539.8 | 366.5 |
| Urari wa huduma | 348.1 | 518.8 | 745.9 | 865.0 | 914.9 |
| Mapato | 422.4 | 581.0 | 827.0 | 970.8 | 985.7 |
| Malipo | 74.4 | 62.3 | 81.0 | 105.8 | 70.8 |
| Urari wa Bidhaa na Huduma | 138.7 | 286.2 | 387.3 | 392.0 | 576.2 |
| Bidhaa na Huduma zilizouzwa nje | 445.6 | 666.3 | 888.5 | 1,037.6 | 1,013.6 |
| Bidhaa na Huduma zilizonunuliwa kutoka nje | 307.0 | 380.1 | 501.2 | 645.7 | 437.4 |
| Urari wa mapato ya vitega uchumi | 4.4 | 3.2 | 42.5 | 68.5 | 99.5 |
| Yaliyoingia | 8.9 | 5.9 | 49.2 | 81.6 | 118.7 |
| Yaliyotoka | 4.5 | 2.7 | 6.7 | 13.1 | 19.2 |
| Urari wa uhamisho mali ya kawaida | 47.7 | 14.7 | 15.7 | 29.7 | 43.4 |
| Iliyoingia | 54.6 | 18.5 | 18.9 | 35.7 | 52.2 |
| Iliyotoka | 6.9 | 3.8 | 3.1 | 6.0 | 8.8 |
| Urari wa Bidhaa, Huduma na Uhamisho Mali | 190.8 | 304.1 | 445.6 | 490.1 | 719.1 |

*Chanzo:* Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania
*Tanbihi: a* inamaanisha takwimu za awali

## Kielelezo 4.11a: Mauzo ya Bidhaa na Huduma Nje ya Nchi kwa Zanzibar


*Dola milioni*




*Chanzo:* Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania

### Kielelezo 4.11b: Uagizaji wa Bidhaa Kutoka Nje kwa Zanzibar

*Dola Milioni*




*Chanzo:* Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki Kuu ya Tanzania


## 4.8 Ukwasi wa Fedha za Kigeni na Viwango vya Kubadilisha Fedha za Kigeni

Mwaka 2024/25, hali ya ukwasi katika soko la fedha za kigeni ilibadilika kuendana na mwenendo wa uchumi wa dunia pamoja na msimu wa mapato ya fedha za kigeni. Kwa robo ya kwanza ya mwaka 2024/25, hali ya ukwasi wa fedha za kigeni ilipungua kufuatia changamoto zilizokumba uchumi wa dunia, japo iliimarika katika robo ya pili, sambamba na kuimarika kwa uchumi wa dunia hususan kupungua kwa bei za bidhaa, utekelezaji wa sera ya fedha iliyolenga kuongeza ukwasi katika nchi zilizoendelea ikiwemo Marekani. Aidha, kuimarika kwa hali ya ukwasi pia kulitokana na ongezeko kubwa la mapato ya fedha za kigeni kutokana na shughuli za utalii, pamoja na mauzo ya dhahabu, korosho, na tumbaku. Vilevile utekelezaji wa sera madhubuti ya fedha, iliyolenga kupunguza ongezeko la mfumuko wa bei kutokana na kupungua kwa thamani ya shilingi dhidi ya fedha ulichangia mwenendo

huu. Hata hivyo ukwasi katika soko la fedha za kigeni ulipungua kidogo katika robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2024/25, kufuatia kukamilika kwa msimu wa mauzo ya mazao nje ya nchi.


Wakati huohuo, thamani ya shilingi dhidi ya dola ya Marekani ilibadilika kuendana na hali ya ukwasi wa fedha za kigeni nchini. Kwa robo ya kwanza ya mwaka 2024/25, shilingi ilishuka thamani, kabla ya kuimarika mwishoni mwa robo ya pili ya mwaka, na baadaye kushuka katika robo ya tatu, japo kwa kasi ndogo ikilinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2023/24 (Kielelezo 4.12a). Kwa wastani, kuanzia Julai 2024 hadi Aprili 2025, thamani ya Shilingi dhidi ya dola ya Marekani katika soko la jumla la fedha za kigeni ilipungua kwa wastani wa asilimia 4.7, ikilinganishwa na asilimia 7.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2023/24. Mwenendo huu pia ulionekana katika soko la rejareja la fedha za kigeni, hali inayoashiria kuendelea kupungua kwa soko lisilo rasmi la fedha za kigeni nchini. Aidha, kiwango cha halisi cha ubadilishaji fedha kinachozingatia uwiano wa biashara baina ya Tanzania na washirika wake wa kibiashara (REER) kilipungua kwa kasi ndogo juu ya mwenendo wake wa muda mrefu mwishoni mwa Aprili 2025 (Kielelezo 4.12b). Hali hii inaashiria kuwa thamani ya shilingi imeendelea kushabihiana na mwenendo viashiria vya kiuchumi, na hivyo kutokuwa na athari za kiushindani kwa bidhaa zinazouzwa nje ya nchi.

## Kielelezo 4.12a: Mwenendo wa Viwango vya Ubadilishaji wa Fedha




*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania

## Kielelezo 4.12b: Kiwango Halisi cha Ubadilishaji wa Fedha




*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania

## 4.9 Mwenendo wa Sekta ya Fedha

Sekta ya fedha iliendelea kuwa thabiti na imara dhidi ya mitikisiko ya muda mfupi, huku viashiria vyote vya msingi vikiwa ndani ya viwango vinavyokubalika. Sekta ya kibenki, ilikuwa na mtaji na ukwasi wa kutosha, na yenye kutengeneza faida, huku ikiendelea kunufaika na matumizi ya mifumo ya kidijitali katika utoaji wa huduma. Uwiano wa mtaji kwa rasilimali (*core capital adequacy ratio*) ulikuwa asilimia 20.2, juu ya ukomo wa chini unaokubalika kisheria wa asilimia 10. Ubora wa rasilimali za benki uliongezeka kufuatia kupungua kwa mikopo chechefu hadi asilimia 3.5 mwezi Aprili 2025, kutoka asilimia 4.1 mwezi Juni 2024. Kiwango hiki kilikuwa chini ya kiwango kinachokubalika na Benki Kuu cha asilimia 5. Mwenendo huu, unatarajiwa kuendelea kuchochea utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi na kupunguza gharama ya ukopaji.

Aidha, Benki Kuu imeendelea kuchukua hatua za kiusimamizi kwa lengo la kupunguza mikopo chechefu, sambamba na kutekeleza sera na maboresho ya kisheria kwa lengo la kudhibiti vihatarishi katika sekta ya benki. Hatua hizo ni pamoja na: (i) kufanya usimamizi na utekelezaji unaozingatia vihatarishi na kuzitaka benki kuboresha viwango vya tathmini katika utoaji wa mikopo; (ii) kuweka mifumo ya kufuatilia utekelezaji wa mikakati ya benki katika kupunguza mikopo chechefu; na (iii) kuzitaka benki kutumia taarifa za wakopaji kutoka katika kanzidata ya taarifa za wakopaji wakati wa kuchakata maombi ya mikopo. Vilevile wafanyakazi wa benki wameendelea kuhimizwa kuzingatia Kanuni za Maadili zilizoandaliwa na Chama cha Benki Tanzania *(Tanzania Bankers Association – TBA*), ikiwa ni miongoni mwa hatua za kuimarisha uadilifu wa wafanyakazi katika sekta ya benki.

## 4.10 Mifumo ya Malipo

Mifumo ya Malipo (SIPS) ikijumuisha Mfumo ya Malipo Makubwa (TISS), Mfumo wa Uhamishaji wa Fedha Kielektroniki (EFT), na Mfumo wa Malipo ya Papo kwa Hapo (TIPS), iliendelea kufanya kazi kwa ufanisi, ikiwa na kiwango cha upatikanaji cha asilimia 99. Aidha, Benki Kuu imeendelea kufanya maboresho katika mifumo hiyo, hususan kwa kutekeleza awamu ya tatu ya TIPS, na kwa kuhamia kwenye viwango vya ujumbe wa ISO20022. Hatua Hizi zinalenga kuongeza ufanisi na uoanifu wa miamala ya ndani na ya kimataifa. Aidha, katika jitihada za kuongeza matumizi ya malipo ya kidijitali na kupunguza utegemezi wa fedha taslimu katika kufanya miamala, Benki Kuu imechukua hatua za ziada kwa kufanya maboresho ya ada za miamala inayofanyika kati ya mifumo oanifu (interoperable transactions), ikiwemo kutoka benki kwenda kwenye akaunti za simu za mkononi na kutoka akaunti za simu kwenda akaunti za benki, kupitia mfumo wa TIPS. Benki Kuu imeweka ukomo wa tozo kwa miamala ambapo kiwango cha juu cha ada ya kuhamisha fedha kupitia mfumo huu haitakiwi kuzidi shilingi 5,000 lengo likiwa ni kuongeza unafuu kwa watumiaji. Kufuatia ukomo huu, benki na watoa huduma za fedha kwa njia ya Kielektroniki *(Electronic Money Issuers – EMIs)* walielekezwa kupunguza ada zao kuendana na muongozo ya Benki Kuu. Sambamba na jitihada hizi, Benki iliendelea kuidhinisha watoa huduma ya mifumo ya malipo, na kufikisha jumla ya kampuni 60 za watoa huduma za kupitia teknolojia ya fedha *(Fintech)* kwa lengo la kuendelea kupunguza utegemezi wa malipo kwa kutumia fedha taslimu nchini, ikiwemo kutoka benki kwenda kwenye akaunti za simu za mkononi na kutoka akaunti za simu kwenda akaunti za benki, kupitia TIPS na hivyo kuongeza unafuu kwa watumiaji.


Matumizi ya mifumo ya malipo ya kidijitali yaliongezeka, ambapo matumizi ya Mfumo wa Uhamishaji wa Fedha wa Kielektroniki *(EFT)* yaliongezeka huku matumizi ya hundi yakipungua. Idadi ya miamala ya EFT iliongezeka kwa asilimia 7.34, huku thamani ya miamala hiyo


ikiongezeka kwa asilimia 16.12. Wakati huohuo, idadi ya miamala ya hundi za shilingi na dola ya Marekani zilizochakatwa kupitia Mfumo wa Malipo ya Hundi *(TACH)* ikipungua kwa asilimia 15.91na asilimia 24.87, mtawalia. Vilevile, thamani ya miamala hiyo ilipungua kwa asilimia 6.03 na asilimia 19.05, mtawalia (Kielelezo 4.13). Kupungua kwa matumizi ya hundi kunatokana na ongezeko la uhamishaji wa fedha kwa njia ya kielektroniki, matumizi ya benki mtandao *(internet banking)*, benki kwa njia ya simu za kiganjani *(mobile banking)*, malipo kwa njia ya simu, pamoja na matumizi ya mifumo mingine ya malipo.

Mifumo ya malipo ya kikanda, ikiwemo Mfumo wa Malipo wa Afrika Mashariki (EAPS) na Mfumo wa Malipo wa ya Papo kwa Hapo wa SADC (SADC-RTGS), iliendelea kufanya kazi kwa ufanisi na kuwezesha kufanyika kwa miamala ndani ya kanda husika. Licha ya uanzishwaji wa mifumo hii, matumizi yake kwa nchi wanachama bado ni madogo, kwa kuangalia idadi na thamani ya miamala. Hali hii inatokana na; kuwepo na sarafu chache za kukamilisha miamala *(settlement)*, mathalani sarafu ya Afrika Kusini (Rand) pekee ndio inatumika katika mfumo wa SADC-RTGS na hivyo kusababisha, ushiriki kubaki kuwa wa benki sita tu za ndani. Aidha katika nchi ya EAC, changamoto ya kutokubalika kwa sarafu za ndani, uelewa mdogo wa mfumo, na viwango tofauti vya maendeleo ya kiuchumi pia vimechangia matumizi madogo ya EAPS. Benki Kuu kwa kushirikiana na benki kuu za EAC na SADC, zinaendelea kutekeleza hatua mbalimbali za kuongeza matumizi ya mifumo hii.

Simu za mkononi zimeendelea kuwa nyenzo kuu katika kuziba pengo kwa wananchi wasiofikiwa na huduma za kifedha kuweza kuzifikia kwa urahisi. Idadi ya miamala kwa njia ya simu iliongezeka kwa asilimia 27.75, huku thamani ya miamala hiyo ikiongezeka kwa asilimia 29.53. Kuongezeka kwa miamala ya fedha kwa njia ya simu kunachangiwa na mazingira wezeshi ya mifumo ya malipo, hususan ada nafuu, kuaminika kwa wateja, na uwepo wa miundombinu ya uhakika (Kielelezo 4.14b).


## Kielelezo 4.13 Miamala ya Hundi





*Chanzo:* Benki Kuu ya Tanzania

**Kielelezo 4.14a: Miamala Katika Mfumo wa Malipo Madogo ya Papo kwa Papo**





Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania


**Kielelezo 4.14b Malipo Kupitia Simu**




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania


## Kielelezo 4.14c: Miamala Katika Mfumo wa Malipo Makubwa (TISS)




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

## Kielelezo 4.14d Miamala ya Kuhamisha Fedha Kielektroniki




Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

# SEHEMU YA TANO

## 5.0 MATARAJIO YA HALI YA UCHUMI

### 5.1 Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia

Uchumi wa dunia unatarajiwa kuwa na mwenendo usioridhisha, ambapo kasi ya ukuaji inatarajiwa kupungua japo kwa viwango tofauti baina ya nchi. Taarifa ya Mwelekeo wa Uchumi wa Dunia *(World Economic Outlook - WEO)* iliyotolewa na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) mwezi Aprili 2025, inakadiria ukuaji wa uchumi wa dunia kupungua hadi asilimia 2.8 mwaka 2025 na asilimia 3.0 mwaka 2026, kutoka makadirio ya asilimia 3.3 kwa miaka yote miwili, mwezi Januari 2025. Vilevile, ukuaji wa uchumi katika nchi zilizoendelea, zinazoibukia kiuchumi, na nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara unatarajiwa kupungua, kutokana na kuongezeka kwa mivutano ya kibiashara hususan kufuatia ongezeko kubwa la ushuru wa forodha kwa bidhaa zinazotoka nje lililofanywa na Marekani na hatua zilizochukuliwa na washirika wake wakuu wa kibiashara, sintofahamu katika sera za kiuchumi na athari za ongezeko kubwa la riba.[4]

Mfumuko wa bei duniani unatarajiwa kupungua, ingawa kwa kasi ndogo kuliko ilivyokadiriwa mwezi Januari 2025 na kufikia asilimia 4.3 mwaka 2025 na asilimia 3.6 mwaka 2026. Aidha, mfumuko wa bei katika nchi zilizoendelea unakadiriwa kuwa juu kidogo mwaka 2025, kulinganishwa na makadirio ya awali, na chini ya makadirio ya awali kwa nchi zinazoendelea na zile zinazoibukia kiuchumi. Hata hivyo, mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kupungua kutokana na matokeo ya utekelezaji wa sera ya fedha iliyolenga kupunguza ukwasi katika nchi nyingi pamoja na mwenendo wa bei za bidhaa muhimu kama

4 Ukuaji wa uchumi katika nchi zilizoendelea unatarajiwa kuwa asilimia 1.4 mwaka 2025, huku katika nchi zinazoibukia kiuchumi na nchi zinazoendelea, ukuaji unatarajiwa kupungua hadi asilimia 3.7 mwaka 2025 na asilimia 3.9 mwaka 2026. Kupungua huku kwa ukuaji kunatokana na madhara makubwa ya hatua za kibiashara za hivi karibuni, hususan kwa nchi zilizoathirika zaidi kama China.


chakula na nishati katika soko la dunia. Mfumuko wa bei unatarajiwa pia kuendelea kupungua katika nchi za EAC na SADC kutokana na utekelezaji madhubuti wa sera za kiuchumi na upatikanaji wa chakula cha kutosha. Aidha, uwezekano wa kupanda kwa mfumuko wa bei ni mdogo, japo mwenendo huu unaweza kuathiriwa na kuongezeka kwa mvutano wa kibiashara au migogoro katika eneo la Mashariki ya Kati. Hata hivyo, sera ya fedha ya benki kuu kwa nchi zilizoendelea, hususan Marekani na Ulaya, inatarajiwa kuweka kipaumbele katika kuchochea ukuaji wa uchumi, hatua inayoweza kupelekea kupunguza riba zao za sera ya fedha.

### 5.2 Mwelekeo wa Uchumi wa Ndani

Uchumi wa hapa nchini unatarajiwa kuendelea kuimarika, licha ya mvutano wa kibiashara unaoendelea duniani. Kwa upande wa Tanzania Bara, uchumi unatarajiwa kukua kwa asilimia 6 mwaka 2025 na asilimia 6.3 mwaka 2026. Mwenendo huu utachagizwa na uwekezaji katika sekta ya umma hususan katika ujenzi wa miundombinu kama reli, barabara, viwanja vya michezo na viwanja vya ndege. Vilevile, uwekezaji katika sekta ya kilimo, hususan miradi ya umwagiliaji, pamoja na hali nzuri ya hewa na sera wezeshi zinazolenga kuongeza uzalishaji katika mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo, utachochea ukuaji wa uchumi. Huduma za kidijitali kupitia simu za mkononi zinatarajiwa kuwa kichocheo kikuu katika utoaji wa huduma za kifedha na bima, huku shughuli za ujenzi zikiendelea kunufaika na ujenzi wa miundombinu unaoendelea. Uchumi wa Zanzibar unatarajiwa kukua kwa asilimia 6.5 mwaka 2025 na asilimia 6.7 mwaka 2026, ukichangiwa zaidi na shughuli za ujenzi—hususan uwekezaji unafanywa na Serikali katika ujenzi wa miundombinu kama barabara, bandari na majengo,pamoja na ongezeko la shughuli za viwanda na utalii.

Mfumuko wa bei hapa nchini unatarajiwa kubaki ndani ya lengo la muda wa kati la asilimia 3-5, ukichangiwa na upatikanaji wa chakula cha kutosha, upatikanaji wa nishati ya uhakika ya umeme na utekelezaji wa sera madhubuti za fedha na za bajeti. Mfumuko wa bei kwa upande wa Zanzibar unatarajiwa kuwa karibu ya asilimia 5, hali inayochangiwa na ongezeko la bei za vyakula, hususan vinavyoagizwa kutoka nje ya nchi pamoja na athari za mabadiliko ya kiwango cha kubadilisha fedha za kigeni. Aidha, uwezekano wa kuongezeka kwa mfumuko wa bei hapa nchini ni mdogo, japo matarajio haya yanaweza kuathiriwa na hali mbaya ya hewa katika maeneo mengi hapa nchini. Vilevile, mwenendo wa sera za biashara duniani na migogoro ya kisiasa vinaweza kusababisha ongezeko la mfumuko wa bei hapa nchini.


**Kielelezo 5.1a: Ukuaji wa Pato la Taifa na Makadirio kwa Tanzania Bara**




*Chanzo:* Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar na Benki Kuu ya Tanzania

## Kielelezo 5.1b: Ukuaji wa Pato la Taifa na Makadirio kwa Zanzibar

Asilimia




*Chanzo:* Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Zanzibar na Benki Kuu ya Tanzania

## SEHEMU YA SITA

## 6.0 SERA YA FEDHA, RIBA NA UBADILISHAJI FEDHA ZA KIGENI 2025/26

### 6.1 Mwelekeo wa Sera ya Fedha

Kulingana na matarajio ya mwenendo wa uchumi pamoja na athari zilizoainishwa, Benki Kuu inatarajia kutekeleza kwa tahadhari sera ya fedha yenye lengo la kuongeza ukwasi kwenye uchumi mwaka 2025/26. Lengo ni kuhakikisha mfumuko wa bei unabaki ndani ya lengo la asilimia 3-5, sambamba na kuwezesha kufikiwa ukuaji wa uchumi wa asilimia 6 mwaka 2025 na asilimia 6.3 mwaka 2026 kwa Tanzania Bara, na asilimia 6.5 na asilimia 6.7 kwa Zanzibar, mtawalia. Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) itakutana kila robo mwaka, kutathmini hali uchumi na mwelekeo wake, na kuamua kiwango cha Riba ya Benki Kuu (CBR) kitakachoendana na malengo ya mfumuko wa bei na ukuaji wa uchumi.

Katika kuboresha maamuzi ya sera ya fedha kwa kuzingatia takwimu, Benki Kuu itaendelea kufanya tafiti mbalimbali na kuhakikisha upatikanaji wa takwimu bora. Tafiti zitakazofanyika zitalenga kuongeza ufanisi wa sera ya fedha. Vilevile, Benki Kuu itaendelea kuelimisha wananchi kuhusu mfumo wa sera ya fedha unaotumia riba ya Benki Kuu, pamoja na umuhimu wa matumizi ya Shilingi katika miamala inayofanyika hapa nchini, ili kuongeza ufanisi wa sera ya fedha katika kufanikisha utulivu wa bei na kuchochea ukuaji wa uchumi. Pamoja na hayo, Benki Kuu itaendelea kufanya maboresho kadhaa yenye lengo la; (i) kuongeza uthabiti wa sekta ya fedha na kupunguza vihatarishi vinavyoambatana na utoaji wa mikopo kwa sekta binafsi, (ii) kuongeza huduma jumuishi za kifedha (kuongeza ufikiwaji wa huduma za kifedha, kuongeza wigo wa huduma za kifedha, kuongeza ufanyaji wa malipo

kwa njia za kidijitali, kuendelea kutoa elimu ya masuala ya fedha kwa wananchi na kumlinda mteja wa huduma za kifedha), na (iii) kuongeza ukwasi na ufanisi wa masoko ya fedha. Utekelezaji wa waraka kuhusu tozo za miamala inayofanyika kati ya benki na mitandao ya simu (e-wallet) kupitia mfumo wa TIPS unatarajiwa kuboresha ufanisi wa sera ya fedha. Vilevile, Benki Kuu itaendelea kufanya maboresho katika mfumo unaotumika kufanya maoteo ya kiwango cha ukwasi nchini na kuchukua hatua za kuongeza uwazi na kupunguza vihatarishi vya ukopeshaji katika soko la fedha baina ya benki, ili kuhakikisha kuwa riba ya mikopo ya siku saba katika soko la fedha kati ya benki inabaki ndani ya wigo wa asilimia +/- 2 ya riba ya Benki Kuu.

### 6.2 Sera ya Riba

Viwango vya riba vitaendelea kuamuliwa kwa nguvu za soko ili kuongeza ufanisi katika upatikanaji wa mitaji hapa nchini. Maamuzi ya Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) kuhusu Riba ya Benki Kuu (CBR) yanategemewa kuongoza upangaji wa riba za mikopo na huduma nyingine za kifedha. Aidha, Benki Kuu kwa kushirikiana na wadau wengine, itaendelea kufanya maboresho katika sekta ya fedha ili kuongeza uwazi katika upangaji wa riba, sambamba na kuongeza usimamizi wa benki na taasisi za huduma ndogo za kifedha, kutanua wigo wa huduma za kifedha na kuongeza elimu ya masuala ya kifedha na utoaji wa taarifa kwa wananchi.

### 6.3 Sera ya Ubadilishaji Fedha za Kigeni na Akiba ya Fedha za Kigeni

Kiwango cha ubadilishaji wa fedha za kigeni kitaendelea kuamuliwa na uwiano wa mahitaji na upatikanaji wa fedha za kigeni katika soko, na hivyo kutumika katika kuukinga uchumi dhidi ya athari zitokanazo na mitikisiko ya uchumi duniani. Kwa mantiki hii, Benki Kuu itashiriki

katika soko la jumla la fedha za kigeni kwa mujibu wa Sera ya Ushiriki wa Soko la Fedha za Kigeni, kwa lengo la; kupunguza mabadiliko makubwa ya muda mfupi katika kiwango cha ubadilishaji wa fedha, kuongeza akiba ya fedha za kigeni, kufanikisha utekelezaji wa sera ya fedha, na kuongeza ukwasi wa fedha za kigeni katika soko. Benki Kuu pia, itaendelea kuhakikisha washiriki wote katika soko la fedha za kigeni wanazingatia kanuni, miongozo na maadili ya ushiriki katika soko hili. Ili kulinda uthabiti wa thamani ya Shilingi, Benki Kuu itaendelea kuhakikisha uwepo wa akiba ya kutosha ya fedha za kigeni, inayotosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa angalau miezi minne kwa mwaka 2025/26. Hii itafanyika kupitia mikakati ya kuongeza akiba ya fedha za kigeni, ikiwemo, mpango wa Benki Kuu wa ununuzi wa dhahabu katika soko la ndani, pamoja na kuingia mikataba ya kubadilishana fedha za kigeni kwa shilingi (foreign exchange swaps) pale itakapobidi.

# VIAMBATISHO

# Jedwali 1: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Tanzania Bara

*Asilimia*

| Shughuli za kiuchumi | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024[a] |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kilimo, misitu na uvuvi | 4.4 | 4.9 | 3.9 | 3.3 | 4.2 | 4.1 |
| Mazao | 4.4 | 5.0 | 3.6 | 2.7 | 4.2 | 4.0 |
| Mifugo | 5.0 | 5.0 | 5.0 | 5.0 | 5.0 | 5.0 |
| Misitu | 4.8 | 3.2 | 3.5 | 3.1 | 4.3 | 3.6 |
| Uvuvi | 1.5 | 6.7 | 2.6 | 1.9 | 1.4 | 2.3 |
| Viwanda na ujenzi | 11.4 | 6.7 | 4.9 | 5.3 | 5.1 | 5.4 |
| Uchimbaji madini na mawe | 17.7 | 7.3 | 9.4 | 10.8 | 11.3 | 8.3 |
| Uzalishaji viwandani | 5.8 | 4.5 | 4.8 | 4.2 | 4.3 | 4.8 |
| Umeme na gesi | 7.2 | 5.5 | 10.0 | 7.6 | 3.9 | 14.4 |
| Maji | 6.9 | 5.8 | 6.5 | 5.5 | 2.5 | 4.1 |
| Ujenzi | 13.3 | 7.8 | 3.3 | 3.9 | 3.5 | 4.1 |
| Huduma | 5.9 | 4.3 | 4.8 | 5.3 | 6.0 | 6.6 |
| Biashara za jumla na rejareja na matengenezo | 4.8 | 2.1 | 3.2 | 3.9 | 4.2 | 4.8 |
| Usafirishaji na uhifadhi mizigo | 8.7 | 8.4 | 3.5 | 3.8 | 4.1 | 4.2 |
| Malazi na huduma ya chakula | 2.6 | -13.7 | 6.7 | 9.0 | 8.3 | 6.0 |
| Habari na mawasiliano | 7.2 | 8.4 | 9.1 | 7.4 | 7.6 | 14.3 |
| Fedha na bima | 4.5 | 3.1 | 4.2 | 9.2 | 14.6 | 13.8 |
| Upangishaji majengo | 4.5 | 4.5 | 4.5 | 4.4 | 4.3 | 4.3 |
| Sughuli za kitaaluma, sayansi na ufundi | 7.6 | 7.3 | 6.8 | 5.8 | 5.5 | 4.8 |
| Huduma zinazohusiana na utawala | 8.4 | 7.8 | 6.9 | 4.6 | 5.0 | 6.2 |
| Usimamizi wa umma na ulinzi | 3.4 | 3.8 | 5.1 | 5.4 | 5.5 | 5.0 |
| Elimu | 6.9 | 3.3 | 5.1 | 5.3 | 6.2 | 6.2 |
| Afya na huduma za jamii | 5.0 | 6.5 | 5.7 | 5.4 | 6.0 | 10.1 |
| Sanaa na burudani | 11.2 | -4.4 | 19.4 | 19.0 | 17.7 | 17.1 |
| Huduma nyingine za kijamii | 6.7 | 5.0 | 8.5 | 5.7 | 6.7 | 5.9 |
| Shughuli za watu binafsi kama waajiri | 3.1 | 3.1 | 3.1 | 3.1 | 3.1 | 2.2 |
| Shughuli zote | 7.1 | 5.2 | 4.6 | 4.8 | 5.3 | 5.6 |
| Kodi za bidhaa | 4.7 | -3.6 | 7.9 | 3.5 | 3.7 | 4.0 |
| Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko | 6.9 | 4.5 | 4.8 | 4.7 | 5.1 | 5.5 |

*Chanzo:* Ofisi ya Taifa ya Takwimu
*Tanbihi:* a inamaanisha takwimu za awali

# Jedwali 2: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Zanzibar

*Asilimia*

| Shughuli za kiuchumi | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024[a] |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Kilimo, misitu na uvuvi | 2.6 | 3.3 | 2.6 | 4.0 | 2.3 | 3.3 |
| Mazao | -5.8 | 1.3 | 2.2 | 6.1 | 2.8 | 6.4 |
| Mifugo | 17.0 | 8.2 | 3.0 | 2.3 | -4.3 | -10.8 |
| Misitu na uwindaji | 3.8 | -4.4 | 4.0 | 2.9 | 6.4 | 0.1 |
| Uvuvi | 3.3 | 3.5 | 2.3 | 3.0 | 8.1 | 14.2 |
| Viwanda | 10.6 | 5.2 | 5.1 | 9.3 | 6.6 | 5.7 |
| Uchimbaji madini na mawe | -1.7 | -6.0 | 9.9 | 9.1 | 10.4 | 17.0 |
| Uzalishaji viwandani | 20.5 | 6.5 | 1.1 | 8.1 | 6.9 | 3.3 |
| Umeme na gesi | 5.2 | -3.2 | 8.0 | 22.3 | 12.4 | 11.2 |
| Maji | 12.9 | 2.0 | 6.9 | 7.0 | 4.6 | 6.3 |
| Ujenzi | 3.1 | 6.5 | 8.9 | 10.2 | 5.5 | 6.3 |
| Huduma | 8.6 | 7.4 | 6.9 | 7.7 | 9.9 | 9.0 |
| Biashara na matengenezo | 9.1 | 1.0 | 14.9 | 4.2 | 12.6 | 11.6 |
| Usafirishaji na uhifadhi mizigo | 4.7 | -6.6 | 9.3 | 3.8 | 9.2 | 0.0 |
| Malazi na huduma ya chakula | 11.5 | -12.7 | 6.6 | 11.7 | 8.2 | 13.7 |
| Malazi | 11.8 | -11.3 | 6.5 | 12.3 | 7.8 | 13.2 |
| Huduma za chakula na vinywaji baridi | 10.0 | -18.9 | 7.5 | 9.0 | 9.8 | 16.3 |
| Habari na mawasiliano | 5.5 | -3.2 | -16.3 | 2.5 | -10.8 | 4.9 |
| Fedha na bima | 3.1 | 2.2 | 9.9 | 3.7 | 54.6 | 13.7 |
| Upangishaji majengo | 6.6 | 6.8 | 7.0 | 7.1 | 7.2 | 7.3 |
| Sughuli za kitaaluma, sayansi na ufundi | -2.9 | 1.1 | 5.0 | 1.4 | 3.5 | 6.6 |
| Huduma zinazohusiana na utawala | 6.9 | -4.6 | 6.6 | -1.5 | 17.0 | 5.9 |
| Usimamizi wa umma | 11.7 | 13.2 | 5.3 | 8.2 | 2.1 | 4.0 |
| Elimu | 7.5 | 9.7 | -0.3 | 9.8 | 3.7 | 7.0 |
| Afya na huduma za jamii | 2.5 | 1.4 | 2.4 | 8.9 | 15.8 | 8.2 |
| Sanaa na burudani | 3.3 | -4.9 | 1.1 | 1.9 | 33.8 | 8.5 |
| Huduma nyingine za kijamii | 2.0 | 12.9 | 6.9 | 6.2 | 8.8 | 7.8 |
| Huduma za ndani | 3.2 | 3.2 | 3.2 | 2.9 | 2.6 | 3.2 |
| Gharama za kifedha zilizojificha (FISIM) | 2.6 | 11.7 | 2.8 | 6.5 | 38.1 | 37.1 |
| Kodi za bidhaa | 1.6 | 1.6 | 1.2 | 3.0 | 5.9 | 7.0 |
| Pato la Taifa (GDP) kwa bei za soko | 7.0 | 1.3 | 5.1 | 6.8 | 7.4 | 7.1 |

*Chanzo:* Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali-Zanzibar
*Tanbihi:* a inamaanisha takwimu za awali

# Jedwali 3: Mfumuko wa Bei kwa Tanzania Bara

Asilimia

| | Uzani (%) | Apr-24 | Mei-24 | Jun-24 | Jul-24 | Ago-24 | Sep-24 | Okt-24 | Nov-24 | Des-24 | Jan-25 | Feb-25 | Mar-25 | Apr-25 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Vyakula na vinywaji baridi | 28.2 | 1.4 | 1.6 | 0.9 | 1.0 | 2.8 | 2.5 | 2.5 | 3.3 | 4.6 | 5.3 | 5.0 | 5.4 | 5.3 |
| Vinywaji vikali na tumbaku | 1.9 | 4.0 | 3.4 | 3.2 | 1.8 | 2.2 | 2.2 | 2.3 | 1.8 | 2.2 | 3.6 | 3.5 | 3.5 | 3.4 |
| Mavazi na viatu | 10.8 | 2.1 | 2.0 | 1.8 | 1.8 | 1.8 | 1.9 | 2.0 | 1.6 | 1.2 | 1.9 | 2.0 | 2.0 | 2.0 |
| Makazi, maji, umeme, gesi na nishati nyinginezo | 15.1 | 5.2 | 5.2 | 6.6 | 6.8 | 5.3 | 5.8 | 5.4 | 4.1 | 2.9 | 2.2 | 3.1 | 3.8 | 3.8 |
| Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa makazi | 7.9 | 3.3 | 3.3 | 3.5 | 3.2 | 1.9 | 2.1 | 2.1 | 2.1 | 2.1 | 2.2 | 2.2 | 2.2 | 2.3 |
| Afya | 2.5 | 2.0 | 2.0 | 1.9 | 1.5 | 1.7 | 1.8 | 1.8 | 1.8 | 1.9 | 1.4 | 1.2 | 1.4 | 1.5 |
| Usafiri | 14.1 | 5.1 | 5.0 | 5.2 | 4.6 | 4.3 | 4.3 | 3.6 | 3.8 | 3.5 | 2.4 | 3.2 | 2.1 | 2.1 |
| Habari na mawasiliano | 5.4 | 1.8 | 1.7 | 1.7 | 1.4 | 1.2 | 1.1 | 1.3 | 1.2 | 1.0 | 0.8 | 0.0 | 0.1 | 0.1 |
| Burudani, michezo na utamaduni | 1.6 | 3.3 | 3.4 | 3.3 | 3.0 | 2.6 | 2.5 | 2.3 | 2.0 | 2.0 | 1.7 | 1.7 | 1.6 | 1.7 |
| Huduma za elimu | 2.0 | 2.8 | 3.3 | 3.4 | 3.4 | 3.3 | 3.1 | 3.1 | 3.1 | 3.2 | 4.5 | 4.2 | 4.1 | 4.1 |
| Migahawa na huduma za malazi | 6.6 | 4.1 | 2.6 | 2.8 | 3.1 | 3.1 | 2.9 | 2.7 | 2.6 | 2.8 | 1.7 | 1.8 | 1.7 | 1.6 |
| Huduma za bima na fedha | 2.1 | 1.5 | 1.6 | 1.7 | 1.0 | 1.0 | 1.3 | 1.3 | 1.2 | 1.1 | 0.8 | 0.7 | 0.7 | 0.8 |
| Usafi binafsi, hifadhi ya jamii na bidhaa na huduma mchanganyiko | 2.1 | 7.5 | 8.2 | 7.2 | 5.9 | 5.6 | 5.7 | 6.4 | 6.3 | 5.3 | 3.1 | 3.3 | 3.3 | 3.0 |
| Fahirisi bidhaa zote | 100.0 | 3.1 | 3.1 | 3.1 | 3.0 | 3.1 | 3.1 | 3.0 | 3.0 | 3.1 | 3.1 | 3.2 | 3.3 | 3.2 |
| Makundi mengine maalumu | | | | | | | | | | | | | | |
| Mfumuko wa bei wa msingi | 73.9 | 3.9 | 3.6 | 3.6 | 3.3 | 3.2 | 3.2 | 3.2 | 3.3 | 2.9 | 2.7 | 2.5 | 2.2 | 2.2 |
| Mfumuko wa bei usio wa msingi | 26.1 | 1.4 | 2.1 | 1.8 | 2.2 | 3.1 | 3.0 | 2.4 | 2.1 | 3.3 | 4.0 | 5.0 | 6.0 | 5.7 |
| Nishati, mafuta na ankara za maji | 5.7 | | | | | | | | | | | | | |
| Huduma | 37.2 | 3.3 | 3.0 | 2.9 | 2.5 | 2.3 | 2.3 | 2.2 | 2.3 | 1.6 | 1.0 | 1.4 | 1.0 | 1.1 |
| Bidhaa | 62.8 | 3.1 | 3.2 | 3.2 | 3.2 | 3.6 | 3.6 | 3.5 | 3.3 | 3.8 | 4.2 | 4.2 | 4.5 | 4.3 |
| Huduma za elimu na bidhaa zinazohusiana na elimu | 4.1 | 3.1 | 3.5 | 3.7 | 3.0 | 2.8 | 3.0 | 2.9 | 3.1 | 2.9 | 4.0 | 4.0 | 4.0 | 3.8 |
| Mfumuko wa bei wa bidhaa zote isipokuwa vyakula na vinywaji baridi | 71.8 | 3.9 | 3.7 | 4.0 | 3.8 | 3.3 | 3.4 | 3.2 | 2.9 | 2.5 | 2.1 | 2.4 | 2.3 | 2.3 |

*Chanzo:* Ofisi ya Taifa ya Takwimu

## Jedwali 4: Mfumuko wa Bei kwa Zanzibar

*Asilimia*

| | Mizania(%) | Apr-24 | Mei-24 | Jun-24 | Jul-24 | Ago-24 | Sep-24 | Okt-24 | Nov-24 | Des-24 | Jan-25 | Feb-25 | Mac-25 | Apr-25 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Mfumuko wa bei wa jumla | 100.0 | 4.9 | 5.3 | 5.7 | 5.3 | 5.1 | 4.8 | 5.8 | 4.5 | 4.9 | 5.3 | 4.8 | 5.1 | 4.3 |
| Mfumuko wa bei wa chakula | 41.9 | 8.0 | 8.9 | 10.6 | 9.0 | 8.9 | 7.3 | 8.2 | 6.6 | 8.1 | 6.6 | 5.8 | 6.4 | 4.1 |
| Mfumuko wa bei wa bidhaa zisizo za chakula | 58.6 | 2.6 | 2.6 | 2.1 | 2.4 | 2.3 | 2.8 | 4.1 | 3.0 | 2.5 | 4.2 | 4.1 | 4.1 | 4.4 |
| Minywaji vikali na tumbaku | 0.2 | 23.8 | 23.8 | 25.4 | 24.6 | 24.7 | 24.7 | 25.1 | 25.9 | 15.4 | 20.1 | 1.0 | -0.3 | -0.3 |
| Mavazi na viatu | 6.3 | 1.3 | 0.1 | 0.7 | 0.7 | 0.3 | 0.2 | 0.0 | 0.6 | 2.1 | 3.0 | 2.8 | 4.2 | 3.9 |
| Makazi, maji, umeme, gesi na nishati nyinginezo | 25.8 | 2.1 | 2.6 | 1.4 | 3.2 | 2.7 | 3.7 | 7.3 | 4.6 | 2.8 | 5.5 | 5.2 | 4.9 | 5.5 |
| Samani, vifaa vya nyumbani na ukarabati wa makazi | 4.8 | 2.9 | 2.6 | 1.8 | 1.5 | 1.4 | 1.5 | 1.3 | 2.0 | 1.7 | 3.3 | 3.6 | 3.4 | 3.4 |
| Afya | 1.3 | -1.5 | -3.4 | -3.2 | -3.1 | -3.1 | -2.4 | -2.1 | -2.4 | -2.4 | -1.7 | -2.0 | -0.4 | 0.3 |
| Usafiri | 9.1 | 4.0 | 4.0 | 3.9 | 3.1 | 2.6 | 2.6 | 1.2 | -0.3 | 1.2 | 1.3 | 1.4 | 1.5 | 2.2 |
| Habari na mawasiliano | 4.2 | 1.4 | 1.5 | 1.5 | 1.6 | 1.7 | 1.7 | 1.7 | 3.3 | 3.5 | 3.4 | 3.3 | 2.8 | 2.0 |
| Burudani, michezo na utamaduni | 1.1 | 4.4 | 4.4 | 4.6 | 4.0 | 4.0 | 4.0 | 3.8 | 3.8 | 4.9 | 3.4 | 3.4 | 3.6 | 4.6 |
| Huduma za elimu | 1.6 | 2.3 | 2.3 | 2.3 | -7.7 | 2.0 | 2.0 | 0.6 | 2.8 | 2.8 | 2.6 | 2.6 | 2.6 | 2.6 |
| Migahawa na huduma za malazi | 1.4 | 11.3 | 11.0 | 11.8 | 11.7 | 11.7 | 15.7 | 15.7 | 15.7 | 13.7 | 0.8 | 0.6 | 0.6 | 0.6 |
| Huduma za bima na fedha | 0.5 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 | 0.0 |
| Usafi binafsi, hifadhi ya jamii na bidhaa na huduma mchanganyiko | 1.7 | 2.9 | 1.6 | 1.6 | 1.6 | 1.6 | 1.6 | 0.3 | 0.8 | 0.8 | 3.3 | 3.5 | 3.6 | 3.5 |

*Chanzo:* Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali-Zanzibar

# Jedwali 5: Takwimu za Kifedha

*Shilingi Bilioni*

| | Apr-24 | Mei-24 | Jun-24 | Jul-24 | Ago-24 | Sep-24 | Okt-24 | Nov-24 | Des-24 | Jan-25 | Feb-25 | Mac-25 | Apr-25 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Rasilimali halisi za nje | 10,089.1 | 10,975.5 | 12,238.3 | 12,226.7 | 13,100.6 | 13,704.3 | 13,773.6 | 13,296.5 | 13,558.2 | 13,242.1 | 14,281.0 | 15,442.1 | 14,658.6 |
| Rasilimali halisi za ndani | 34,229.9 | 34,117.4 | 34,523.8 | 34,704.7 | 34,591.9 | 34,360.2 | 35,469.4 | 36,221.2 | 35,346.8 | 36,592.4 | 36,309.7 | 36,699.8 | 38,679.1 |
| Mikopo kwa sekta binafsi | 33,757.6 | 33,983.9 | 34,980.8 | 35,354.6 | 35,730.9 | 36,174.1 | 36,517.8 | 36,741.8 | 36,097.4 | 36,576.1 | 36,982.5 | 37,999.3 | 38,755.8 |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) | 44,319.0 | 45,092.9 | 46,762.1 | 46,931.4 | 47,692.5 | 48,064.6 | 49,243.0 | 49,517.7 | 48,905.0 | 49,834.5 | 50,590.7 | 52,141.9 | 53,337.7 |
| Amana za fedha za kigeni (FCD) | 10,493.7 | 10,846.0 | 11,496.1 | 11,450.8 | 11,998.8 | 12,427.9 | 12,745.0 | 12,345.2 | 11,765.3 | 12,419.3 | 12,794.3 | 13,605.9 | 13,846.3 |
| *Amana za fedha za kigeni (Dola milioni)* | *4,080.0* | *4,190.0* | *4,400.8* | *4,330.9* | *4,479.0* | *4,609.6* | *4,697.0* | *4,670.7* | *4,829.2* | *5,095.5* | *4,995.4* | *5,183.8* | *5,187.0* |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) | 33,825.3 | 34,246.9 | 35,266.0 | 35,480.6 | 35,693.7 | 35,636.6 | 36,498.0 | 37,172.5 | 37,139.7 | 37,415.2 | 37,796.4 | 38,536.0 | 39,491.4 |
| Ujazi wa fedha, kwa tafsiri finyu (M1) | 20,263.3 | 21,093.0 | 21,995.8 | 22,176.0 | 22,085.9 | 21,825.4 | 22,273.8 | 22,817.1 | 22,905.5 | 23,073.0 | 22,984.8 | 23,541.7 | 24,013.1 |
| Fedha zilizo kwenye mzunguko | 6,146.7 | 6,521.8 | 7,076.5 | 7,085.6 | 7,302.0 | 7,353.5 | 7,408.2 | 7,597.1 | 7,351.6 | 6,997.7 | 6,926.3 | 7,190.0 | 7,024.1 |
| Amana za hundi | 14,116.6 | 14,571.2 | 14,919.3 | 15,090.3 | 14,783.8 | 14,471.9 | 14,865.6 | 15,219.9 | 15,553.9 | 16,075.4 | 16,058.5 | 16,351.7 | 16,989.0 |
| Viashiria vingine | | | | | | | | | | | | | |
| Fedha Taslimu | 10,066.6 | 11,046.4 | 10,926.3 | 10,896.5 | 11,053.1 | 11,133.7 | 11,765.8 | 11,859.0 | 12,024.5 | 11,670.3 | 12,053.8 | 11,793.1 | 11,878.9 |
| Akiba za benki | 2,835.7 | 3,533.2 | 2,886.6 | 2,663.7 | 2,730.7 | 2,667.0 | 3,176.7 | 3,233.1 | 3,351.5 | 3,516.5 | 4,041.6 | 3,623.1 | 3,738.7 |
| Fedha zilizo nje ya Benki Kuu ya Tanzania | 7,230.9 | 7,513.2 | 8,039.7 | 8,232.8 | 8,322.3 | 8,466.7 | 8,589.1 | 8,625.8 | 8,672.9 | 8,153.8 | 8,012.2 | 8,169.9 | 8,140.2 |
| Wastani wa Fedha Taslimu | 10,305.9 | 10,556.7 | 11,040.0 | 10,896.5 | 11,053.1 | 11,223.1 | 11,568.7 | 11,755.6 | 11,988.7 | 11,988.7 | 11,767.1 | 12,138.7 | 11,779.6 |
| Kiwango cha ubadilishaji fedha (mwisho wa kipindi) (Shilingi ya Tanzania/Dola Milioni) | 2,572.0 | 2,588.5 | 2,612.2 | 2,644.0 | 2,678.9 | 2,696.1 | 2,713.4 | 2,643.1 | 2,436.3 | 2,437.3 | 2,561.2 | 2,624.7 | 2,669.4 |
| Viwango vya ukuaji wa kila mwaka (%) | | | | | | | | | | | | | |
| Fedha Taslimu | 6.4 | 15.2 | 0.7 | 6.9 | 6.4 | 12.0 | 19.8 | 17.8 | 19.1 | 12.1 | 18.9 | 15.8 | 18.0 |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) | 10.9 | 12.2 | 10.9 | 10.1 | 10.6 | 11.4 | 14.6 | 13.6 | 11.1 | 13.9 | 15.1 | 17.1 | 20.3 |
| Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) | 8.9 | 9.3 | 8.2 | 8.1 | 7.2 | 6.6 | 9.1 | 11.2 | 9.2 | 10.8 | 11.7 | 12.9 | 16.8 |
| Mikopo kwa Sekta Binafsi | 17.6 | 16.5 | 17.2 | 17.6 | 16.7 | 17.5 | 17.0 | 15.3 | 12.4 | 12.8 | 13.2 | 14.0 | 14.8 |

*Chanzo*: Benki Kuu ya Tanzania

## Jedwali 6: Riba za Masoko ya Fedha na Mitaji

Asilimia

| Aina ya riba | Apr-24 | Mei-24 | Jun-24 | Jul-24 | Ago-24 | Sep-24 | Okt-24 | Nov-24 | Des-24 | Jan-25 | Feb-25 | Mac-25 | Apr-25 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Riba katika soko la fedha baina ya mabenki | | | | | | | | | | | | | |
| Siku 1 (Overnight) | 6.51 | 7.02 | 6.92 | 6.80 | 7.62 | 7.88 | 7.74 | 7.73 | 7.07 | 7.69 | 7.87 | 7.91 | 7.90 |
| Siku 2-7 | 7.04 | 7.35 | 7.40 | 7.42 | 7.83 | 8.26 | 8.17 | 8.11 | 7.38 | 7.74 | 8.02 | 8.02 | 7.98 |
| Riba ya jumla | 7.02 | 7.34 | 7.36 | 7.24 | 7.79 | 8.16 | 8.04 | 8.06 | 7.41 | 7.80 | 8.06 | 8.12 | 8.00 |
| Riba ya mikopo ya siku 1 kati ya mabenki na Benki Kuu *(Lombard rate)* | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 | 8.00 |
| Riba ya mikataba ya mauziano ya dhamana za muda mfupi *(Reverse REPO rate)* | 6.57 | 6.57 | 6.57 | 6.57 | 7.88 | 8.00 | 8.00 | 7.72 | 6.26 | 7.21 | 7.21 | 7.21 | 7.21 |
| Riba ya dhamana za serikali | | | | | | | | | | | | | |
| Siku 182 | 8.45 | 8.22 | 6.57 | 6.57 | 7.30 | 7.30 | 8.17 | 8.30 | 8.30 | 8.20 | 8.20 | 8.20 | 8.47 |
| Siku 364 | 10.38 | 7.83 | 6.75 | 8.84 | 10.63 | 10.98 | 11.66 | 12.78 | 12.95 | 12.63 | 11.99 | 10.11 | 8.92 |
| Riba ya jumla | 10.33 | 7.86 | 6.75 | 8.81 | 10.61 | 10.85 | 11.55 | 12.68 | 12.95 | 12.51 | 11.93 | 10.10 | 8.86 |
| Riba za hati fungani za serikali | | | | | | | | | | | | | |
| Miaka miwili | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 11.64 | 12.55 | 12.55 | 12.08 |
| Miaka mitano | 10.09 | 10.09 | 10.09 | 10.09 | 10.09 | 10.09 | 12.41 | 12.41 | 12.41 | 12.41 | 12.41 | 13.14 | 13.14 |
| Miaka saba | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 | 9.71 |
| Miaka kumi | 12.30 | 12.30 | 12.30 | 12.30 | 13.26 | 13.26 | 13.26 | 13.26 | 13.26 | 14.08 | 14.08 | 14.08 | 14.26 |
| Miaka kumi na tano | 13.66 | 15.16 | 15.16 | 15.05 | 15.05 | 15.35 | 15.76 | 15.76 | 15.76 | 15.76 | 15.76 | 14.63 | 14.63 |
| Miaka ishirini | 15.24 | 15.24 | 15.13 | 15.17 | 15.40 | 15.45 | 15.76 | 15.64 | 15.71 | 15.71 | 15.28 | 15.28 | 15.11 |
| Miaka ishirini na tano | 16.13 | 16.13 | 15.38 | 15.38 | 15.38 | 15.42 | 15.42 | 15.93 | 15.93 | 15.84 | 15.84 | 15.84 | 15.84 |
| Riba ya Benki Kuu | 6.00 | 6.00 | 6.00 | 6.00 | 6.00 | 6.00 | 6.00 | 6.00 | 6.00 | 6.00 | 6.00 | 6.00 | 6.00 |

*Chanzo*: Benki Kuu ya Tanzania

# Jedwali 7: Riba za Benki

*Asilimia*

| Aina ya riba | Apr-24 | Mei-24 | Jun-24 | Jul-24 | Ago-24 | Sep-24 | Okt-24 | Nov-24 | Des-24 | Jan-25 | Feb-25 | Mac-25 | Apr-25 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A: Shilingi ya Tanzania | | | | | | | | | | | | | |
| Riba za amana | 2.79 | 2.87 | 2.86 | 2.87 | 3.02 | 2.84 | 2.85 | 2.69 | 2.84 | 2.97 | 2.98 | 2.86 | 2.89 |
| Riba za jumla za amana za | | | | | | | | | | | | | |
| muda maalum | 7.44 | 7.65 | 7.66 | 8.15 | 7.98 | 8.20 | 8.25 | 8.18 | 8.33 | 8.31 | 8.13 | 8.00 | 7.82 |
| Miezi sita | 9.12 | 9.37 | 9.25 | 9.09 | 8.91 | 9.15 | 9.30 | 9.19 | 9.30 | 9.86 | 9.40 | 9.68 | 9.36 |
| Mwaka mmoja | 8.21 | 8.97 | 9.09 | 9.01 | 8.82 | 9.12 | 10.41 | 9.63 | 9.62 | 10.08 | 9.48 | 8.14 | 9.27 |
| Riba za amana za wateja wakubwa | 9.33 | 9.72 | 9.86 | 9.96 | 10.12 | 9.88 | 10.27 | 10.14 | 10.39 | 11.80 | 11.40 | 10.35 | 10.52 |
| Riba za mikopo za Jumla | 15.42 | 15.47 | 15.30 | 15.29 | 15.26 | 15.54 | 15.67 | 15.67 | 15.71 | 15.73 | 15.14 | 15.50 | 15.16 |
| Muda mfupi (Hadi mwaka 1) | 15.93 | 15.98 | 15.57 | 15.67 | 15.50 | 15.67 | 16.06 | 15.56 | 15.74 | 15.70 | 15.77 | 15.83 | 16.15 |
| Muda wa kati (Mwaka 1 hadi 2) | 15.77 | 15.82 | 15.69 | 15.49 | 15.50 | 15.97 | 16.25 | 16.93 | 16.79 | 16.89 | 16.06 | 16.56 | 16.33 |
| Muda wa kati (Miaka 2 hadi 3) | 15.87 | 15.88 | 15.78 | 16.06 | 16.09 | 16.26 | 16.48 | 16.36 | 16.21 | 16.35 | 15.53 | 16.44 | 15.25 |
| Muda mrefu (Miaka 3 hadi 5) | 15.44 | 15.50 | 15.37 | 15.21 | 15.14 | 15.20 | 15.06 | 15.17 | 15.24 | 15.25 | 14.09 | 14.32 | 13.88 |
| Riba za mikopo za wateja wakubwa | 13.95 | 12.69 | 12.82 | 12.78 | 12.79 | 12.92 | 12.93 | 12.77 | 12.83 | 12.80 | 13.42 | 12.94 | 12.88 |
| B: Fedha za kigeni | | | | | | | | | | | | | |
| Riba za amana | | | | | | | | | | | | | |
| Amana za akiba | 0.79 | 0.90 | 0.97 | 0.53 | 1.28 | 0.91 | 0.73 | 0.71 | 0.81 | 0.90 | 0.76 | 0.77 | 0.53 |
| Riba za jumla za amana za | | | | | | | | | | | | | |
| muda maalum | 3.77 | 3.65 | 3.91 | 3.97 | 3.73 | 3.68 | 3.85 | 3.99 | 4.20 | 4.22 | 3.66 | 2.98 | 2.94 |
| Miezi sita | 4.39 | 4.46 | 4.38 | 3.74 | 4.40 | 4.54 | 4.59 | 4.44 | 4.36 | 3.89 | 4.11 | 3.81 | 3.55 |
| Mwaka mmoja | 4.49 | 4.40 | 4.44 | 4.26 | 3.89 | 3.21 | 3.83 | 3.57 | 3.54 | 3.62 | 3.88 | 3.50 | 3.01 |
| Riba za mikopo za Jumla | 8.10 | 8.19 | 7.23 | 8.34 | 8.56 | 8.44 | 8.77 | 8.53 | 8.80 | 8.83 | 8.97 | 8.93 | 8.89 |
| Muda mfupi (Hadi mwaka 1) | 8.74 | 8.77 | 6.58 | 9.10 | 9.55 | 9.41 | 9.50 | 9.50 | 9.44 | 9.89 | 9.93 | 9.99 | 9.97 |
| Muda wa kati (Mwaka 1 hadi 2) | 7.94 | 7.89 | 7.10 | 7.48 | 7.69 | 6.75 | 7.60 | 7.74 | 7.78 | 7.58 | 7.64 | 7.94 | 8.16 |
| Muda wa kati (Miaka 2 hadi 3) | 8.47 | 8.27 | 7.63 | 8.31 | 8.28 | 8.70 | 8.76 | 8.02 | 9.19 | 8.81 | 8.57 | 8.28 | 8.23 |
| Muda mrefu (Miaka 3 hadi 5) | 6.94 | 6.94 | 6.56 | 7.35 | 7.41 | 7.52 | 8.23 | 8.01 | 8.23 | 8.18 | 9.11 | 8.61 | 8.36 |

*Chanzo*: Benki Kuu ya Tanzania

**Jedwali 8: Ratiba ya Vikao vya Kamati ya Sera ya fedha kwa mwaka 2025/26**

| Robo mwaka | Tarehe ya Mkutano wa Kamati | Siku ya Kutangaza maamuzi ya Kamati na Muhtasari kwa Vyombo wa Habari |
|---|---|---|
| Robo ya Kwanza | 2 Julai, 2025 (Jumatano) | 3 Julai, 2025 (Alhamisi) |
| Robo ya Pili | 1 Oktoba, 2025 (Jumatano) | 2 Oktoba, 2025 (Alhamisi) |
| Robo ya Tatu | 7Januari, 2026 (Jumatano) | 8 Januari, 2026 (Alhamisi) |
| Robo ya N ne | 1 Aprili, 2026 (Jumatano) | 2 Aprili, 2026 (Alhamisi) |

*Tanbihi:* Tarehe zilizoainishwa zinaweza kubadilika pale itakapobidi.

Kwa maelezo zaidi wasiliana na:
Benki Kuu ya Tanzania, Barabara ya 16 ya Jakaya Kikwete 40184,
Sanduku la Posta 2303, Dodoma, Tanzania
Simu: +255 26 296 3182-7 au +255 22 223 2541
Barua Pepe: botcommunications@bot.go.tz
Tovuti: https://www.bot.go.tz